# Nipashe

Jumatatu Aprili 10, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581276

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



MID WEEK JACKPOT!
TZS. 544,830,140
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




## Adaiwa kujinyonga kisa madeni

UKURASA 5




UKURASA 11

# Maaskofu wakemea ufisadi

## • Matumizi mabaya ya madaraka... pia ndoa za jinsia moja...*Ukurasa 2*



"Katika maandiko alikuwapo mwanafunzi mmoja wa Yesu aitwaye Yusufu wa Arimathaya, huyu alikuwa ni mtu mwenye uwezo mzuri kiuchumi, mtu tajiri ,ndiye aliyepewa mwili wa Yesu akauzike baada ya kuuomba kwa Pilato, wakati huo akina Petro (mwanafunzi wa Yesu) hawaonekani, kwa hiyo tusiwachukie matajiri," **Dk. Kimaro.**



"Wale ambao wanaendelea kuliibia taifa sio kwamba hawaelewi, bali nafsi zao zimeshikwa na roho ya kuturudisha kwenye huzuni," **Dk. Malasusa.**

"Rushwa ni adui wa haki na tukitaka kudumu katika amani katika taifa letu kila mmoja atende kwa haki, tukitenda kwa haki tutakuwa tunadumisha amani na utulivu, haki huzaa amani na hutokana na Mungu," **Askofu Kisare**





"Waumini wayaishi maagizo ya Yesu Kristo kwa kutenda yaliyo mema na kuwa waadilifu, ili kumpa Mungu nafasi ya kutekeleza majukumu yake kwao,"**Ruwaichi.**

"Utajiri hauji bila ya kufanya kazi, lakini baadhi ya Watanzania wanapenda kutafuta utajiri kwa njia za mkato," **Sangu.**



## RIPOTI CAG:

# Mshtuko ghala la pembe za ndovu

UKURASA 3

# 'Sauna sababu moja chanzo cha ugumba'

UKURASA. 4


MICHEZO **KAZE ALIA KIWANGO KIBOVU YANGA FA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Maaskofu wakemea ufisadi

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wa dini nchini wameonyesha kukerwa na taarifa za wizi na matumizi mabaya ya madaraka kunakodaiwa kufanywa na viongozi na watumishi wa umma waliopewa dhamana ya kuisaidia nchi.

Aidha, wamesema Rais Samia Suluhu Hassan asiwaonee aibu waliotajwa kwenye ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwa kuwa wanaliteketeza taifa huku wananchi wakiendelea kuteseka.

Viongozi hao waliyasema hayo kwa nyakati tofauti wakati wa Ibada ya Sikukuu ya Pasaka ambayo waamini wa dini ya Kikirsto wanaungana ulimwenguni kukumbuka kufufuka kwa Yesu Kirsto.

**UFISADI**

Askofu Mkuu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Alex Malasusa, aliwataka waamini kuendelea kuwaombea viongozi waliopewa dhamana na huku wao wakienenda kinyume na maadili ya utumishi wao, ikiwamo kuliibia taifa.

Alisema viongozi wanaobeba dhamana ya kuongoza sio kwamba hawajui wanachokitenda kwa kuwa udhaifu wao katika uaminifu, unalenga kulirudisha taifa nyuma hivyo maombi ni msingi na nafsi zao zitabadilika na kutambua kuwa vitendo wanavyovitenda havimpendezi Mungu. Askofu Malasusa, aliyasema hayo jana, kwenye ibada ya kwanza ya Sikukuu ya Pasaka iliyofanyika katika Kanisa la Azania Front, jijini Dar es Salaam.

"Tunapoanza kusikia wenzetu ambao walipewa wajibu wa kutunza mali za nchi yetu, fedha za nchi yetu, wako ambao tena wanaturudisha kwenye huzuni wanahitaji kuombewa.

"Wale ambao wanaendelea kuliibia taifa sio kwamba hawaelewi, bali nafsi zao zimeshikwa na roho ya kuturudisha kwenye huzuni. Yesu ambaye amesamehe, akutane na watu hawa ili uaminifu, uadilifu iwe desturi katika familia na taifa.

"Anatukumbusha sisi wa leo kuliona tendo hili la kufufuka, kuimarisha imani yetu ya kikristo. Ikiwa Kristo asingefufuka imani hii ingekuwa bure. Kufufuka kwa Yesu ni kuhakikishiwa ushindi ametuondolea uoga dhidi ya kifo, ukifa ndani ya Yesu.

"Hata leo kuna watu tunaishi kama Masadukayo, maisha kana kwamba tutaishi milele mtu anayeishi katika dhambi, Yesu amemlinganisha na maiti. Kufufuka kwa Yesu ni ushindi dhidi ya dhambi alisema Askofu Malasusa.

Kadhalika, aliwataka waamini wote wanaosherehekea Sikukuu ya Pasaka, wapate ujasiri na neema ya kujua dhambi na kwamba waikemee, akisema licha ya kwamba wakati mwingine hatua hiyo husababisha marafiki kumtenga mkemeaji dhambi.

"Mkristo lazima uikemee dhambi, tumepewa jukumu la kuwa nuru na kumulika mahali pote. Dunia imeingia kwenye giza, watu wanajaribu kutafuta furaha, kuna mambo mengi yanayomfurahisha mwanadamu, lakini bado hajaipata furaha.

"Hakuna asiyejua wanavyotaka kubadilisha mpango wa Mungu katika uumbaji, tulipoanza miaka ya 2000 tukawa na majadiliano makubwa juu ya ndoa ya jinsia moja. Kanila la Kilutheri limekemea ndoa za jinsia moja, sheria, mila za Tanzania hazikubali ndoa za jinsia moja.

"Si kwamba hayakuwapo, yalikuwapo tangu enzi za Sodoma na Gomora, lakini yalishtua zaidi yalipoingia katika kanisa. Najaribu kupiga picha kwa sasa Mungu anatuangaliaje wanadamu uumbaji wake aliweka utaratibu utaendelezwa na mwamume, na mwanamke," alieleza Askofu Malasusa.

"Kuna mambo ya msingi ya mwanadamu hata kama hayawezi kuzungumzwa, lakini hayawezi kutokea. Haya mambo ya ndoa za jinsia moja ni mambo ya nuru na giza, omba, ili giza litokomee, hata yasikufikirishe," alisisitiza Askofu Malasusa.

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga Mhashamu Liberatus Sangu, akihubiri katika ibada hiyo katika Kanisa la Ngokolo, aliwaonya Watanzania kutafuta utajiri kwa njia za mkato kwa wizi pamoja na ufisadi hali ambayo imekuwa ikisababisha machafuko nchini, ikiwa ni pamoja na mauaji hata kumsahau Mungu na kutenda yasiyostahili.

Alisema utajiri hauji bila ya kufanya kazi, lakini baadhi ya Watanzania wanapenda kutafuta utajiri kwa njia za mkato, na hata kukimbilia kwenye ramli chonganishi ambazo husababisha mauaji, au kwenda kwenye imani zingine kukanyangwa vichwa wakiaminishwa watapata nyumba na magari.

**UTENDAJI WA RAIS SAMIA**

Askofu wa Kanisa la ACTS Felloship Tanzania, Dk. Mpeli Mwaisumbe, akitoa salamu za Pasaka alisema kazi iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ni kubwa na utendaji wake unaridhisha na kwamba anapaswa asiowaonee haya vigogo waliotajwa kwenye Ripoti ya CAG).

Dk. Mwaisumbe alisema kuwa mbali ya taifa kuendelea kujivunia mafanikio makubwa ambayo yameletwa na serikali, bado kuna mambo yanakwenda ndivyo sivyo na kila mmoja anawajibu wa kukemea kwa nguvu zote.

"Hivi karibuni imetoka ripoti ya CAG na katika ripoti hiyo kuna watu wametajwa kuhusika na matumizi mabaya ya fedha za umma, fedha ambazo kama zingetumika vizuri zingesaidia kuleta maendeleo kwenye taifa hivyo bila kuangalia sura ya kiongozi ni vizuri zikarejeshwa ili zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo," alisema na kuongeza:

"Rais wetu mama Dk. Samia amekuwa mfano mwema wa uongozi kwenye taifa na hata Bara la Afrika, hivyo tunahitaji kumuunga mkono wote kwa nguvu zetu zote sisi viongozi wa dini tuendelee kumuombea afya njema ila na wale walioopo serikalini wanaomsaidia wawe waadilifu wa fedha za umma," alisisitiza.

Akizungumzia maadili katika jamii, Askofu Dk. Mpeli alisema ni wajibu wa jamii kuendelea kukemea vitendo vya ushoga na usagaji vinavyoendelea kuchipua katika jamii kwa kuwa vitendo hivyo ni chukizo mbele za Mungu na kila mzazi ama mlezi ana wajibu wa kutoa elimu kwa watoto wake ili kuepukana na vitendo viovu vya ndoa za jinsia moja .

**RUSHWA**

Askofu Mkuu wa Kanisa Mennonite Tanzania (KMT), Nelson Kisare, aliwataka waumini kujitakasa na kuachana na matendo mabaya kwenye jamii vikiwamo vitendo vya rushwa.

Alikemea pia mapenzi ya jinsia moja akieleza kwamba kanisa hilo linapinga vitendo hivyo kwa kuwa ni kinyume na mpango wa Mungu.

Akizungumza Dar es Salaam jana katika Ibada ya Sikukuu ya Pasaka iliyofanyika Makao Makuu ya Kanisa hilo Upanga, Askofu Kisare alisema amani haiwezi kutawala kama kuna baadhi ya watu wanaonewa.

"Rushwa ni adui wa haki na tukitaka kudumu katika amani katika taifa letu kila mmoja atende kwa haki, tukitenda kwa haki tutakuwa tunadumisha amani na utulivu, haki huzaa amani na hutokana na Mungu," alisema askofu Kisare.

Alimpongeza Rais Samia kwa kuunda tume ya kuangalia namna ya kuboresha taasisi za Haki Jinai nchini, akieleza kwamba hatua hiyo inadhihirisha ujasiri wa kuimarisha mifumo ya haki.

"Tujisafishe mioyoni mwetu kutokana na matendo yetu mabaya kupitia neno la Mungu linalosafisha dhambi tunajua dunia ya leo kuna mambo yanaendelea kinyume na Mungu na matendo ya ukatili dhidi ya watoto na manyanyaso mengi yanayoendelea kwa wajane na yatima," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana wa Kanisa hilo, Amos Masanja, alisema kupitia sikukuu hiyo ni wakati wa watu wote kujitakasa kwa kuacha maovu na kumkimbilia Yesu.

Muumini wa kanisa hilo, Mary Meso, alisema kupitia injili jamii inaweza kuondokana na matendo mabaya ya mmomonyoko wa maadili hivyo wanapaswa kuzingatia wito wa Yesu kwa kutenda mema.

Jackson Masawe, muumini kwenye kanisa hilo, aliwataka wakristo wote kuendelea kutenda mema kama ilivyokuwa kwenye mfungo wa kwaresma.

Askofu wa Kanisa Aglikana Tanzania Dayosisi ya Central Tanganyika Dk. Dikson Chilongani, aliwataka viongozi wa juu wa serikali kuhakikisha wanapambana na vitendo vya rushwa ambavyo vinaonekana kushamiri zaidi.

Alisema kuwa nchi haiwezi kuwa na maendeleo ya kiuchumi kama haitapambana na kuzuia vitendo vya rushwa kwani rushwa ni dhambi na inapotosha haki.

**MATAJIRI**

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) dayosisi ya Kijitonyama Dar es Salaam, Dk. Eliona Kimaro ameitaka jamii kutokuwa na chuki na watu wenye uwezo mkubwa kiuchumi badala yake wawathamini na kuwatia moyo wa kutoa zaidi, ili jamii inufaike na utajiri wao kuliko kuwaita majina mabaya.

Akizungumza na waumini wa kanisa hilo katika Ibada ya Pasaka ya usharika huo jana, alisema ipo tabia ya watu kuwachukia watu wenye uwezo mkubwa kiuchumi (matajiri) na kuwafanyia visa bila sababu za msingi na kuwataka waache tabia hiyo kwa kuwa inawavunja moyo na kuwafanya kwenda kuwekeza mahali pengine.

"Katika maandiko alikuwepo mwanafunzi mmoja wa Yesu aitwaye Yusufu wa Arimathaya, huyu alikuwa ni mtu mwenye uwezo mzuri kiuchumi, mtu tajiri ,ndiye aliyepewa mwili wa Yesu akauzike baada ya kuuombwa kwa Pilato, wakati huo akina Petro (mwanafunzi wa Yesu) hawaonekani, kwa hiyo tusiwachukie matajiri," alisema Dk. Kimaro.

**MAISHA UADILIFU**

Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mhashamu Yuda Thadeus Ruwa'ichi aliwasihi wanaumini wa kanisa hilo kuyaaishi maagizo ya Yesu Kristo kwa kuwa kutenda yaliyo mema na kuwa waadilifu ili kumpa Mungu nafasi ya kutekeleza majukumu yake kwao. Askofu wa Jimbo Katoliki Moshi, mkoani Kilimanjaro, Mhashamu Ludovick Minde, amesema tabia iliyojitokeza ya kubadili jinsia (transgender) sio mpango wa Mungu na kwamba badala yake ni udhalilishaji dhidi ya kazi nzuri ya uumbaji aliyoifanya Mwenyezi Mungu.

Akitoa salamu za Sikukuu ya Pasaka katika Seminari ya Kibosho alisema, "tabia hii ni sehemu ya mmomonyoko wa maadili ambayo yanadhalilisha Sakramenti Takatifu ya ndoa na Heshima ya ndoa aliyoiweka Mungu na chakusikitisha vijana wamekuwa mstari wa mbele kuendekeza dhambi hii."

***Imeandikwa na Christina Mwakangale, Restuta James, Jenifer Gilla, Halfani Chusi na Enock Charles (DAR), Marco Maduhu (SHINYANGA) Francis Godwin (IRINGA), Mary Mosha (MOSHI) na Paul Mabeja (DODOMA).**



Askofu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa akiwatakia heri ya Pasaka, waumini baada ya Ibada ya Pasaka katika Usharika wa Azania Front, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ... abaini fedha za hospitali kushikiliwa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imeonyesha kuwa fedha za hospitali, zenye thamani ya Sh. bilioni 20.66 zinashikiliwa licha ya kukosekana kwa dawa na vifaa tiba.

Aidha, CAG katika ukaguzi wake, amebaini upotevu kadhaa wa mapato, ikiwa ni pamoja na kukataliwa kwa madai ya bima, yenye thamani ya Sh. bilioni 7.8.

Hasara ambayo ilipatikana kutokana na dawa zilizoisha muda wake, zenye thamani ya Sh. bilioni 2.24 na Sh. milioni 703 katika misamaha inayotolewa kwa wagonjwa wasiostahili.

Katika ripoti hiyo, CAG Charles Kichere, alibaini pia kuwapo kwa wataalamu wa afya 289, wanaotoa huduma bila kuwa na leseni halali, ununuzi wa dawa na vifaa tiba, vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.75 bila ya uhakiki wa kutosha na malipo ya dawa na vifaa tiba, ambavyo havikuwasilishwa, vyenye thamani ya Sh. bilioni 16.85.

"Ukaguzi pia ulibaini kuwa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 4.56 vilinunuliwa, lakini havikutumika na kulikuwa na ucheleweshaji wa ujenzi wa majengo ya hospitali, yenye thamani ya Sh. bilioni 74.15.

"Mwishowe nilibaini kuwapo kwa mtiririko wa taarifa zisizolingana, kati ya GoT-HoMIS, Afyacare, na GePG ndani ya mamlaka ya hospitali hiyo," alifafanua CAG Kichere.

Aprili 6, mwaka 2023, Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alitimiza matakwa ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Tanzania, kwa kuiwasilisha Ripoti ya CAG bungeni jijini Dodoma, ikiwa na ripoti 22.

Wakati, Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Mwaka 2021/2022 iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imebaini kuwa kwa kipindi cha miaka sita (2016/17 hadi 2021/22), Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya, ilitoa Sh. milioni 85, kwa ajili ya usimamizi shirikishi kupitia timu za usimamizi wa afya za halmashauri, sawa na asilimia mbili ya makusanyo ya ada ya Sh. bilioni 3.599. Lakini hata hivyo, halmashauri 14 zilizotembelewa hazikupokea fedha hizo.

Aidha, ripoti hiyo ya ufanisi inaonyesha CAG amebaini kiwango cha chini cha ukaguzi wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya.

Alisema ukaguzi ulibaini kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2021/22, Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya, haikufanya ukaguzi kwa asilimia 70 ya vituo binafsi vya afya vilivyosajiliwa nchini, kinyume na mpango mkakati wake wa miaka 2016/17- 2020/21. Kwa mujibu wa CAG, vituo vya huduma za afya vilivyokaguliwa, vilikuwa kati ya asilimia 10 na 52.

**BARAZA WAFAMASIA**

Vilevile, CAG alisema Baraza la Wafamasia, halikufanya ukaguzi wa maduka ya dawa katika vituo binafsi na hiari vya huduma za afya.

"Ukaguzi ulibaini kuwa, Baraza la Wafamasia halikukagua maduka yote ya dawa yaliyosajiliwa katika vituo binafsi na hiari vya afya, ikiwa pamoja na maeneo ya kutolea dawa yaliyoidhinishwa, kama ilivyoainishwa katika mpango mkakati wake wa mwaka 2016/17 hadi 2021/22.

"Zaidi, ilibainika kuwa vituo vyote 132 vilivyotembelewa katika halmashauri 14 nchini havikufanyiwa ukaguzi na Baraza la Wafamasia.

"Kutokaguliwa kwa maduka ya dawa na sehemu zilizoidhinishwa kutoa dawa kunaweza kusababisha kutozingatiwa kwa kanuni na viwango, hivyo kuhatarisha usalama wa wagonjwa. Hali hii ilitokana na kukinzana kwa majukumu ya udhibiti wa vituo binafsi vya huduma za afya, ambapo jukumu la Baraza la Ufamasia ni kusajili tu maduka ya dawa yanayojiendesha na si maduka ya dawa yaliyoambatanishwa katika vituo vya huduma za afya. "Maduka ya dawa yaliyoambatanishwa na vituo vya huduma za afya yanatathminiwa na kuendeshwa kwa wakati mmoja na uanzishaji wa vituo vya huduma za afya unaofanywa na Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya. Hali hii inalizuia Baraza la Wafamasia, ambalo ndilo lenye dhamana ya kufanya na utaalamu wa kukagua wafamasia kwa ajili ya usajili wa maduka ya dawa."




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akimkabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 23 mshindi wa Mashindano ya Qur-aan Afrika, Omar Mohamed kutoka nchini Misri (katikati), yalioandaliwa na Taasisi ya Al-Hikma Foundation na kudhaminiwa na Benki ya PBZ, katika Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam jana. Wa (tatu kushoto) ni Shekhe Mkuu, Mufti Abubakar bin Zuberi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CAG: Mshtuko ghala la pembe za ndovu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MALI bila daftari huisha bila habari! Ni msemo wenye maana kwamba ni vyema kuweka kumbukumbu za vitu vyako katika mahali pa usalama na katika mpangilio mzuri au kupangilia kazi zako kwa ufasaha zaidi ili kukuwezesha kujua, kutambua kwa urahisi mwenendo mzuri wa kazi zako.

Wakati kukiwa na angalizo hilo la wahenga, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini tatizo katika utunzaji wa taarifa za pembe za ndovu kwenye ghala la serikali.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/22 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa wiki iliyopita, CAG Charles Kichere, amebaini kuwa moto uliodaiwa kuteketeza ghala la pembe za ndovu mwaka 2013, haukuchunguzwa. CAG Kichere alisema alibaini kuwa mwaka 2013 kulikuwa na tukio la moto kwenye ghala la pembe za ndovu ambalo lilisababisha kupotea kwa taarifa muhimu zinazohusiana na pembe za ndovu zilizohifadhiwa.

"Jambo la kushangaza ni kuwa hakuna uchunguzi uliofanyika ili kubaini chanzo cha moto huo na madhara yake hadi wakati wa ukaguzi.

"Nilibaini kutopatikana kwa taarifa sahihi za pembe za ndovu zilizohifadhiwa kwa ajili ya kufanya tathmini na kuzipima upya pembe hizo za ndovu, hali isiyoridhisha ya pembe zote zilizohifadhiwa kiasi cha kusababisha kuharibika kwa ubora na hadhi yake na kushindwa kuhuisha rejista juu ya hali na thamani za pembe za ndovu," anabainisha.

CAG pia anasema amebaini programu iliyotumika kurekodi na kusajili akiba ya pembe za ndovu na nyara zingine haijaunganishwa na seva kuu ya programu ya wizara kwa sababu programu hiyo ilikuwa imepitwa na wakati, baadhi ya pembe za ndovu zilikosa taarifa zake za maandishi, huku nyingine zikiwa na taarifa zisizosomeka kutokana na ubovu wa paa la kuhifadhia uliosababisha kuvuja kwa paa hilo.

Anataja kasoro zingine zinajumuisha zana za kuwekea alama zilizotumiwa kurekodi taarifa juu ya pembe za ndovu ziliandikwa kwa wino unaoweza kufutika, na kuzifanya zifutike kwa urahisi na ghala la kuhifadhia lilikuwa katika hali mbaya kutokana na kuwa na nafasi ndogo, paa kuvuja, hewa chafu, mazingira machafu, umeme usio imara, ukosefu wa kamera na vifaa vya kuzima moto.

"Kwa maoni yangu, ukosefu wa udhibiti sahihi wa pembe za ndovu unaweza kusababisha upotevu wa taarifa zinazohusiana na pembe za ndovu, taarifa hizi ni muhimu katika kesi za kisheria dhidi ya ujangili na juhudi nyingine zinazolenga kudhibiti vitendo vya ujangili," CAG anatoa angalizo.

Anabainisha kuwa Menejimenti ya Wizara imethibitisha kuwapo upungufu huo na itafanya uhakiki wa nyara kila baada ya miaka mitatu hadi minne, kulingana na upatikanaji wa rasilimali.

"Napendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii iweke mfumo madhubuti wa kudhibiti na kusimamia pembe za ndovu.

"Pia, iandae mfumo madhubuti wa kuhifadhi kumbukumbu za taarifa zote zinazohusiana na pembe za ndovu, ukiwamo mpango mkakati wa taarifa za upotevu kutokana na matukio yasiyotarajiwa kama vile moto," CAG anawasilisha hoja yake.

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**PASCAL GEORGE MASELE**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC.740 CBF,** yenye Engine No. **156FMI-5A*D2F42161*** aina ya **HAUJUE.** Yeyote atakayeiona ataoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **WMB/RB/614/2021.**

# 'Sauna sababu moja chanzo cha ugumba'

**Na Christina Mwakangale**

VIJANA hususan wanaume walio kwenye umri wanaotarajia kupata watoto, wameshauriwa kupunguza au kuacha kabisa matumizi ya kuoga katika sauna ikielezwa kuwa kiwango cha joto kwenye bafu hilo ni moja ya sababu za ugumba.

Kadhalika, madereva wa bodaboda wakiwamo waendesha vyombo vya moto mbalimbali kwa muda mrefu, ambavyo injini yake ipo jirani na mfumo wa uzazi wa mwanaume, wamo hatarini.

Sauna ni bafu la mvuke kwenye chumba kidogo au jengo lililosanifiwa kama sehemu ya kupata joto la mvuke, ambao huweza kuwa mkavu au wenye maji maji, na huwa na kiwango cha joto 150 ° F hadi 195 ° F (65 ° C hadi 90 ° C).

Bingwa wa Uzazi na Magonjwa ya Wanawake kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Belinda Balandya, alitoa tahadhari hiyo hivi karibuni, jijini Dar es Salaam, kwenye semina kuhusu afya, iliyoandaliwa na Wakfu wa Merck Foundation, ambayo ni tawi la Merck KGaA la Ujerumani.

Alisema kuna sababu tofauti zinazosababisha wenza wanaotarajia kupata mtoto, kuchukua kipindi cha mwaka mmoja bila matarajio, kuwa hali hiyo kitaalamu hutafsiriwa kuwa ni ugumba.

Vile vile, alisema mara kadhaa suala la ugumba jamii hudhani limeegemea kwa wanawake pekee na kwamba elimu duni ni sababu ya tatizo hilo, akilitaja huchangia pia na wanaume.

"Dawa za kupulizia kwenye mboga na zikaliwa ndani ya muda mfupi, kuliko inavyoshauriwa kuna uhusiano na tatizo la ugumba. Dereva bodaboda na wanaooga kwa sauna wanaohitaji watoto wanashauriwa kuwa makini iwapo bado ni vijana wanaohitaji watoto.

"Kundi hilo (dereva) lipo hatarini kwa kuwa hukaa juu ya injini (ya pikipiki) kwa muda mrefu na joto kali kwa saa nyingi na wanaotumia sauna ambao umri wao bado vijana wanashauriwa kutumia 'shower' (maji ya bomba la mvua) kuliko kukaa kwenye sauna muda mrefu," alisema Dk. Belinda akiongeza: "Nilikuwa na client (mgonjwa) mmoja ambaye alipata ajali akiwa anaendesha gari, alikuwa na presha sana na hakukubali hapo awali, hadi baadaye alipokubali kuanza matibabu."

Akifafanua zaidi kuhusu ugumba, Dk. Belinda alisema, tatizo hilo huwafanya wanaokumbwa nalo kuwa na msongo, jinsi zote, kwa kuwa baadhi ya jamii huwanyanyapaa, hasa mwanamke kunyanyapaliwa kutokana na kutopata ujauzito.

"Sio wanawake tu ambao wana tatizo hili. Wanaume pia mfano kama anavaa boxer (nguo ya ndani) na sehemu ya maumbile ya viungo vya uzazi wa kiume kubanwa sana ni tatizo," alisema Dk. Belinda.

"Tunahitaji kuongeza elimu, kuhusu hili, kunahitajika elimu watu wawe na lishe bora, kupunguza msongo," alisisitiza.

Naye Bingwa wa Wanawake na Uzazi, Dk. Nicholaus Mazuguni kutoka hospitali ya Avinta Care, mkoani Arusha, alisema sababu zipo nyingi za watu kukosa mtoto huku mwanamume akishindwa kumpa mimba mwanamke na mwanamke kushindwa kupata mimba.

Alitaja sababu mojawapo ni mbegu hafifu na dhaifu kwa upande wa mwanamume, unywaji pombe uliokithiri na matumizi ya tumbaku na mwanamke ni makovu kwenye kizazi, uvimbe na kutokuwamo uwiano wa vichocheo vya mwilini.

"Mwanamke utaenda 'period' (siku za hedhi) lakini sio uhakika kwamba utashika mimba, mirija kuziba, inaweza kuwa tatizo. Mwanamume huchangia asilimia 30 ya ugumba na mwanamke kwa kiwango hicho hicho cha asilimia 30 na asilimia 10 sababu hazieleweki," alisema Dk. Nicholaus.

"Tunahitaji elimu katika jamii ili kuepukana na unyanyapaa dhidi ya ugumba, ukatili kwa wanawake. Kuna imani potofu, kuna stori nilikutana nayo mwanamke aliambiwa anywe damu ya period yake ili apate mtoto," alisema bingwa huyo.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akishiriki Ibada ya Jumapili ya Sikukuu ya Pasaka, katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Mpango ahadharisha wazazi matumizi simu watoto wao

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewataka wazazi kuwa makini na watoto hususani kwenye matumizi ya simu za mkononi, ikiwamo kuchunguza wanaangalia vibonzo vya aina gani.

Pia, amewataka kufuatilia na kuchunguza marafiki wanaoambatana na watoto wao ikiwamo kuzingatia malezi yenye maadili mema.

Dk. Mpango alisema hayo jana kwenye Ibada ya Sikukuu ya Pasaka iliofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa, jijini hapa, wakati akitoa salamu za Pasaka kwa waamini na taifa.

Dk. Mpango alisema wazazi wanapaswa kusimamia kwa ukaribu masuala ya malezi ya watoto hususani wa kiume kutokana na mambo machafu yanayoendelea mitaani na maeneo mbalimbali.

Alisema hivi sasa kila mmoja ana simu janja ambazo ndizo chanzo cha vijana wengi kuharibika kutokana na mambo mbalimbali wanayoangalia na kuwataka wazazi wawe makini kuwafuatilia ikiwamo kuwachunguza marafiki wanaoandamana kwenye mizunguko yao.

"Wazazi kuweni makini na malezi ya watoto chunguzeni marafiki waliokuwa nao na mjitahidi kulea watoto katika mazingira mazuri yenye kumpendeza Mungu," alisisitiza.

Alisema imefika wakati wanaume kwa wanaume wanaoana au wanawake kwa wanawake wanaoana huku akionya kuwa mambo hayo hayakubaliki mbele ya mwenyezi Mungu hata maadili hayaruhusu kufanya hivyo.

Alisema zamani watoto wa kike ndio walikuwa wanalindwa na kuchungwa, lakini kutokana na mambo kubadilika, wazazi wanapaswa kuzingatia malezi na ulinzi kwa watoto wa kiume ambao huharibika kutokana na utandawazi.

Alisisitiza suala la wazazi kuwapeleka watoto kanisani kujifunza masuala ya dini ambayo ni muhimu, akitolea mfano kufurahishwa na Shirika la Utoto Mtakatifu ambalo watoto hufundishwa mambo ya Mungu.

Pia, walimu, masista na viongozi wa dini wasiache kukemea mambo hayo kwa nguvu zote kwa sababu hayakubaliki kidini wala lwa utamaduni wa Tanzania.

Aliipongeza Parokia ya Kiwanja cha ndege kutokana na kutunza mazingira huku akisisitiza jamii kuendelea kutunza mazingira kwa kupanda miti kila mahali.

# Kero barabara eneo uwekezaji yatatuliwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

HATIMAYE kero ya barabara katika eneo la uwekezaji la Zegereni inatarajiwa kumalizika Julai, mwaka huu utakapokamilika mradi wa ujenzi wa kilomita 12.5 kwa kiwango cha lami.

Zegereni ni kati ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda na kwa muda mrefu barabara hiyo imekuwa kikwazo kwa wananchi na wawekezaji kwa kutopitika vizuri hususani kipindi cha mvua.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA), Mkoa wa Pwani, Mhandisi Leopold Runji alisema, kukamilika kwa barabara hiyo kutawezesha wawekezaji kusafirisha malighafi na bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda hivyo kwa urahisi.

Aliyaeleza hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Visiga-Zegereni-Misugusugu.

Alisema barabara hiyo ilianza kujengwa Machi 2022 na Mkandarasi China Railway Seventh Group inatarajiwa kukamilika Julai 20, kwa gharama ya Sh. bilioni 16.8.

Alisema ujenzi umefikia asilimia 75 na tayari mkandarasi amelipwa Shilingi bilioni nane na kwamba kwasasa vipo viwanda vikubwa 31 na eneo lingine la uwekezaji la ekari 1,200 limepimwa kati ya 5,297 zilizopo Zegereni.

"Serikali iliahidi kutatua vikwazo kwa wawekezaji na hili linaendelea kufanyika katika kongani hii ya Zegereni sasa tatizo la barabara linaenda kumalizika na kuwawezesha wawekezaji kusafirisha bidhaa zao bila kikwazo," alisema.

Mhandisi Runji alisema ujenzi wa barabara kiwango cha lami kwenye maeneo ya uwekezaji inafanyika pia katika eneo la Kwala ilipo kongani ya viwanda, zilitumika Sh. bilioni tano kujenga kilomita tano.

Said Kondo na Clemence Joseph wakazi wa Zogowale inapopita barabara ya lami Visiga- Zegereni hadi Misugusugu, wameishukuru serikali kwa ujenzi wa barabara hiyo ambayo awali ilikuwa ya vumbi na kupitika kwa shida.

Walisema kabla ya ujenzi wa barabara hiyo usafiri wa bodaboda walilipa Sh. 3,000 hadi 4,000 kutoka Zogowale hadi Visiga tofauti na sasa wanalipa Sh. 1,500 na pia wenye nyumba za kupanga wameongezeka baada ya kuwa na barabara ya uhakika.

Naye Radhia Ismail alisema ujenzi wa barabara hiyo umeanza kuleta mabadiliko kiuchumi kwa wafanyabiashara zao kwa kuwa gharama za usafirishji zimepungua, pia watu wanaofika katika maeneo hayo wamezidi kuongezeka.

## HABARI KITAIFA

# Ajitoa uhai kisa madeni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Kijiji cha Itwangi, wilayani Shinyanga, Ally Hamis (48), amekutwa katika chumba chake akiwa amejinyonga huku akiacha ujumbe uliokuwa ukionesha madeni aliyokuwa anadaiwa.

Imeelezwa kuwa tukio hilo lilitokea Aprili 8 na ujumbe uliokutwa kwenye chumba chake ulibainisha baadhi ya madeni yake ambayo ni pamoja na Sh. 40,000 za baiskeli, Sh. 300,000 alizokuwa akidaiwa na baba yake mdogo na deni la debe moja la mahindi. Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alisema lilitokea majira ya saa mbili asubuhi na baada ya kupokea taarifa hizo, askari polisi walifika eneo hilo na kukuta mwili wa marehemu ukiwa unaning'inia ndani ya nyumba yake pamoja na ujumbe huo wa madeni.

"Chanzo cha tukio hili huenda ni msongo wa mawazo kutokana na madeni ambayo alikuwa anadaiwa, pia mwili wa marehemu umeshafanyiwa uchunguzi na daktari na umekabidhiwa kwa ndugu zake kuendelea na shughuli za mazishi," alisema Magomi. Mwenyekiti wa Kijiji cha Itwangi, Kisendi Lubinza, akiongea na gazeti hili kwa njia ya simu alisema kuwa katika ujumbe marehemu aliandika kuwa ameamua kujiua mwenyewe na asihusishwe mtu yeyote, sababu nyigine pia kaamua kumfuata mama yake mzazi ambaye alishatangulia mbele ya haki.

Kamanda aliwaasa wananchi kijiji hicho wanapokabiliwa na matatizo wafike kwenye uongozi wa kijiji kutafuta namna ya kulitatua, na sio kubaki nalo rohoni na kusababisha kuchukua maamuzi ambayo hugharimu maisha yao.




Mtoto mwenye umri unaopaswa kuwa shule, akisafisha kioo cha gari katika Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mwenge Dar es Salaam hivi karibuni, ili ajipatie riziki. Mamlaka zinazohusika zinatakiwa kuchukua hatua kutokana na ongezeko kubwa la watoto wa mitaani. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Zaidi mil. 632/- mradi EP4R nyaraka zake zaungua

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini kuwa zaidi ya Sh. milioni 632.5 za Mradi wa Programu ya Kutekeleza Elimu kwa Matokeo Awamu ya Pili (EP4R), zilizotumika kujenga Chuo cha Ualimu Sumbawanga, hazina nyaraka za malipo.

Kwa mujibu wa ripoti iliyowasilishwa mwishoni mwa wiki na CAG, Charles Kichere, ukaguzi wa mradi huo unaotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, haukuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi ya Sh. 632.5.

Kwa mujibu wa CAG, fedha hizo ni kati ya Sh. bilioni 2.51 zilizotumika katika ujenzi wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga, mkoani Rukwa.

"Nilitaarifiwa kwamba hati za malipo na nyaraka zinazohusiana na matumizi haya zilipotea katika ajali ya moto iliyotokea Desemba 25, moto huo uliunguza nyaraka zinazohusiana na mradi huo," alisema

Aprili 6, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia Waziri wa Fedha na Mipango, alitimiza matakwa ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Tanzania, kwa kuiwasilisha Ripoti ya CAG bungeni jijini Dodoma, ikiwa na ripoti 22.

Baada ya ufafanuzi kuhusu ripoti hizo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (LAAC), Nangenjwa Kaboyoka, alisema baada ya kuchambua na kutoa maazimio ya Bunge, Rais Samia Suluhu Hassan, atapelekewa ili achukue hatua.

"Tukishapeleka mapendekezo bungeni sasa Bunge ni jukumu lake kuyachukua kama maazimio ambayo yanapelekwa kwa rais ambaye ndiye mwenye mamlaka ya uteuzi ili wale watakaokuwa wamebainika katika ubadhirifu huu mkubwa wa fedha za umma ndiye atakayechukua hatua," alisema Kaboyoka.

# Merck Foundation kuongeza ufadhili wa madaktari

**Na Christina Mwakangale**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Merck Foundation Afrika, Seneta Dk. Rasha Kelej, amesema Taasisi hiyo itaongeza wigo wa ufadhili wa mafunzo kwa madaktari wa Tanzania ili kuongeza fursa ya upatikanaji wa huduma za kibingwa na bobezi nchini.

Taasisi ya Merck Foundation ambayo ni tawi la Shirika la Merck KGaA la Ujerumani, imekwishatoa mafunzo kwa watoa huduma sekta ya afya 1,500 barani Afrika, kati yao 33 ni madaktari wa Kitanzania tangu kuanzishwa kwake mwaka 2017.

Dk. Rasha, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, wakati wa sherehe za kuwatuza wanahabari wanane wa Tanzania walioshinda tuzo zinazotolewa na Taasisi hiyo, akisema madaktari nchini wana nafasi ya kuomba ufadhili wa mafunzo kwa kuwa dirisha la kupokea maombi limefunguliwa.

"Nimefurahi kukutana nanyi nyote leo na kuweza kujadiliana namna ambavyo programu zetu zimeweza kusaidia jamii zenu na natazamia kwa siku zijazo zitaleta manufaa zaidi kwa jamii zenu kiujumla," alisema Dk. Rasha.

Alisema Merck Foundation itahakikisha inaimarisha na kuboresha afya na kufikia malengo na kusaidia wananchi wa barani la Afrika, ikiwamo kutambua mchango mkubwa wa vyombo vya habari kutokana na kuinua kiwango cha uelewa kuhusu haki ya elimu ya msichana na kupinga vitendo vya ukatili.

"Tumeshafadhili madaktari 33 wa Tanzania na sasa wamebobea katika eneo la uchunguzi na matibabu ya magonjwa mbalimbali ikiwamo saratani, kisukari pamoja na tatizo la ugumba na upandikizaji mimba.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Samwel Rweyemamu aliushukuru wakfu huo, akisema programu hiyo imekuja kwa wakati muafaka.

"Uchunguzi kwa matibabu dhidi ya magonjwa ya moyo bado ni suala jipya Tanzania, tunaona kuna idadi kubwa ya watu wanaokabiliwa na magonjwa haya, tunazidi kuimarisha mifumo yetu ya uchunguzi na tiba.

"Utoaji elimu hasa kuepukana na unene pamoja na magonjwa ya kuambukiza itasaidia kuondokana na magonjwa, natoa wito kwa wataalamu wa afya kujiunga na programu za Merck foundation ili kuongeza ujuzi," alisema bingwa.

Aidha, Mwenyekiti wa Bodi ya E. Merck KG na Merck Foundation Bodi ya Wadhamini, Prof. Dk. Frank Stangenberg-Haverkamp, alisema wakfu huo umeongeza uelewa na kuwajengea uwezo wanataaluma tofauti ikiwamo wanasayansi na wanahabari.

"Mtakubaliana na mimi kwamba kuna maendeleo makubwa tangu tulipoanza kutoa ufadhili kwa madaktari mnamo mwaka 2018. Juhudi hizi zimesaidia kuwajengea uwezo na bila shaka mmeweza kuimarisha afya ya jamii nchini Tanzania.

"Tunatazamia kuendeleza ushiriki wetu katika ufadhili wa programu hii ya kuwajengea uwezo madaktari wa Tanzania. Madaktari wa Tanzania watanufaika na ufadhili wa masomo kwa ngazi ya ubingwa na ubobezi katika nyanja ya uchunguzi na matibabu dhidi ya magonjwa mbalimbali," alisema Prof. Frank.

Aidha, Prof. Frank na ujumbe wake, walikutana na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na kufanya mazungumzo, kuhusu wakfu huo unavyotoa huduma kwa wataalamu wa afya pamoja na wanahabari.

Ummy aliwashukuru Merck Foundation kwa ufadhili wa kuwasomesha Madaktari Bingwa na Ubingwa Bobezi katika fani mbalimbali ikiwamo magonjwa ya wanawake na NCDs.

Wakfu huo, umejikita kuboresha afya na ustawi wa watu pamoja na kuendeleza maisha yao kupitia sayansi na teknolojia na kutoa ufadhili wa masomo kwa madaktari, huku nchi 50 barani Afrika ikiwamo Tanzania, Liberia, Gambia, Burundi, Malawi, Sierra Leone, Zambia, Zimbambwe, Guinea, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Nepal, Bangladesh na zingine.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga kujiaminisha tu hakutoshi, jipangeni CAF

**BADO** mijadala ya nani ana wakati mgumu na mwepesi kuelekea mechi za robo fainali kwenye michuano ya kimataifa kwa wawakilishi wa nchi, Simba na Yanga, imekuwa mingi na kuingia hadi kwa wachezaji, baada ya droo ya hatua hiyo kufanyika wiki iliyopita jijini Cairo, Misri.

Simba ambao ni wawakilishi wa nchini kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, wengi wanaona hapo ndio mwisho wa safari kwa msimu huu baada ya kupangwa kukutana na Wydad Casablanca ya Morocco ikianzia nyumbani Uwanja wa Benjamin Mkapa Aprili 21 kabla ya kwenda kumalizia ugenini Aprili 28, mwaka huu.

Kwa upande wa Yanga inayoiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, yenyewe itaanzia ugenini nchini Nigeria dhidi ya Rivers United Aprili 23, na mechi ya marudio itakuwa Aprili 30, mwaka huu Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mashabiki na wachambuzi wengi wa soka nchini wamekuwa wakiiona Simba ina mlima mrefu kupanda zaidi ya Yanga kwa kuwa tu imepangwa na Wydad ambao ni mabingwa watetezi, lakini pia wakiwa kwenye ubora wa hali ya juu ukilinganisha na kiwango cha Wekundu wa Msimbazi hao. Kingine kinachowafanya kuipa nafasi Simba kutolewa ni kutokana na hatua ya makundi ya michuano hiyo kufungwa nyumbani na ugenini na wapinzani wakubwa wa Wydad katika Ligi ya Morocco, Raja Casablanca, jambo ambalo wanaamini dhahama hiyo itawakuta tena. Kwa upande wa Yanga, pia wanaamini inaweza kusonga mbele kwa kuwa ina kikosi bora zaidi msimu huu ukilinganisha na msimu uliopita wakati Rivers United wakiwatoa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa kwa jumla ya mabao 2-0, wakishinda 1-0 ugenini na ushindi kama huo nyumbani.

Dhana hiyo pia imeingia hadi kwa baadhi ya wachezaji wa Yanga wakijigamba kwamba wanakwenda kulipa kisasi cha msimu uliopita kutolewa na Wanigeria hao, jambo ambalo ni nzuri kama watajikita katika mbinu watakazopewa na walimu wao na juhudi binafsi uwanjani, lakini kinyume cha hapo, mambo yanaweza kuharibika. Kwa ujumla sisi tunaamini hakuna timu iliyo rahisi wala ngumu katika michuano hii, hasa inapofika hatua kama hii ya mtoano, hivyo kinachotakiwa ni kujiandaa zaidi kimbinu na kujua namna ya kucheza mechi hizi za mtoano, ambazo huhitaji ushindi mkubwa na kujua mbinu za kuulinda.


Rivers United, ambayo wengi wanaamini ni timu nyepesi nayo ilianzia raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kama Yanga, kabla ya kuangukia Kombe la Shirikisho zilipo sasa, ikiwa huko ilifanikiwa kutinga raundi ya kwanza ambapo ilipangwa kucheza na wapinzani wa Simba wajao, Wydad Casablanca.

Katika mchezo wa kwanza, ikiwa nyumbani Nigeria, Rivers United ilishinda mabao 2-1, kabla ya mchezo wa marudiano nchini Morocco kuchapwa 6-0, hivyo kuangukia Kombe la Shirikisho na Wydad kusonga mbele, hivyo Yanga haipaswi kujidanganya kwamba Wanigeria hao ni wepesi kihivyo, ama Simba kuiona Wydad ni wagumu sana. Yanga ikibweteka, Rivers United inaweza kupata ushindi mkubwa nyumbani na hali ikawa ngumu katika kupindua matokeo zitakaporudiana, lakini na Simba ikijipanga inaweza kushinda Uwanja wa Benjamini Mkapa na ikienda Morocco ikang'ang'ania sare, yote yanawezekana.

Kikubwa ni wawakilishi hao wa nchi kila mmoja kuchukulia mechi hizo kama ngumu na zinazohitaji kufanya maandalizi ya kutosha ya kupambana kwa jasho nyumbani na ugenini ili kupata ushindi, na si mechi za kusubiri kushinda nyumbani pekee, kwani hujui mpinzani wako amejipangaje anapokuwa ugenini.

Tunachotaka ni kuona wawakilishi wetu hao wakisonga mbele hatua ya nusu fainali na hatimaye fainali, na hilo haliwezi kutokea kwa hofu wala kuamini tu mpinzani wako ni mwepesi, bali maandalizi ya kina na kisaikolojia yanapaswa kuanza sasa kabla ya mechi hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# 'Dabi' Simba, Yanga isogezwe mbele zijiandae michuano CAF

Na Adam Fungamwango

**RATIBA** ya Ligi Kuu Tanzania Bara inaonyesha kuwa Aprili 16, mwaka huu kuna mechi kati ya watani wa jadi, Simba na Yanga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Siku zote inapochezwa 'dabi' hiyo ya Kariakoo huwa hakuna dogo, hata kama ikiwa ni mechi ya kirafiki. Wachezaji watatumia nguvu zao zote, uwezo na kila kitu walichonacho kuhakikisha wanaibuka na ushindi.

Kwa bahati mbaya sana mechi hii imekuja vibaya kwani timu hizi zote zipo kwenye michezo ya kimataifa.

Zamani ingewezekana kabisa kuwa moja ingekuwa imeshatolewa, au zote mbili, lakini safari hii kwa mara ya kwanza Simba na Yanga zipo kwenye hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa.

Simba ipo Ligi ya Mabingwa na Yanga Kombe la Shirikisho. Simba itacheza na Wydad Casablanca ya Morocco, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Aprili 21 na kwenda kumalizia ugenini Aprili 28, wakati Yanga imepangwa kucheza dhidi ya Rivers United ya Nigeria, ikianzia ugenini Aprili 23, na mechi ya marudio itakuwa Aprili 30, mwaka huu Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Hapa utaona baada ya dabi kupigwa, Simba itakuwa na siku tano tu kucheza dhidi ya Wydad na Yanga itakuwa na siku saba. Tena afadhali Simba itakuwa ikicheza nyumbani, lakini Yanga ina siku hizo ikiwa inasafiri kwenda ugenini, hivyo haitakuwa na muda kabisa wa kupumzika.

Tunajua mechi za dabi wachezaji wanavyotumia nguvu, halafu mechi ikiisha wanaanza safari kwenda kucheza mechi nyingine ngumu, hii inaweza kuwaathiri na kupoteza mechi kirahisi.

Kwa sababu wachezaji watakuwa na uchovu wa dabi na wa safari pia. Hata wachezaji wa Simba haitokuwa rahisi kwao kwani watakuwa na mechi mbili ngumu, kucheza dhidi ya Yanga, halafu wiki inayofuata kuwavaa Mabingwa Watetezi wa Afrika si jambo la mchezo. Binafsi, ningeshauri Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kuisogeza mbele mechi hiyo kwa maslahi mapana na si ya Simba na Yanga tu, bali kwa soka la Tanzania.

Kwa miaka zaidi ya 20, hatujawahi kuziona Simba na Yanga zote zikiwa kwenye hatua za makundi mechi za kimataifa, lakini safari hii siyo makundi tu, kizazi hiki kimeshuhudia zikifika hadi robo fainali, hivyo ni jambo la fahari kubwa kwa TFF na nchi kwa ujumla.

Inawezekana lisijitokeze tena, hivyo TFF na Bodi ya Ligi ilichukulie jambo hili kwa umakini mkubwa, kuahirisha na kuisogeza mbele mechi hiyo ili kuzipa nafasi timu hizo kujiandaa na mechi zao za kimataifa.

Itawapa nafasi hata viongozi wa klabu hizo kujiandaa kwa umakini zaidi na kuondokana na presha za mechi za dabi. Kwa sasa ni kama watakuwa wamechanganyikiwa mechi ili wajiandae vizuri zaidi ya nyingine, na makocha pia watakuwa na wasiwasi wa kuumia kwa wachezaji wao, kuwapumzisha pia inakuwa tatizo.

Hata hivyo, kwa utamaduni wa mechi hizi, huwezi kumpumzisha mchezaji muhimu kwenye mechi za Simba na Yanga eti kwa ajili ya mechi ya kimataifa.

Hapa sasa inatakiwa Bodi ya Ligi ya TFF kuzisaidia timu hizi ili zifanye maandalizi sahihi na kwa ubora unaotakiwa ili kuzipa uwezo wa kufanya vema kwenye mechi zao za robo fainali kwa faida ya soka la Tanzania na nchi kwa ujumla.

Tumeona vyama vya soka, Tunisia, Morocco, na Guinea vikizisaidia timu zao zilizoshiriki Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho kwa kuahirisha mechi zao kadhaa ili kuzipa nafasi ya kujiandaa kikamilifu.

Ikiwa haitofanya hivyo, kuna wasiwasi wa timu zetu kuondoshwa kutokana na uchovu wa mechi hiyo ngumu, safari, lakini pia hata timu moja ikifungwa mechi ya dabi, haitokuwa vizuri kisaikolojia kuanzia wachezaji, viongozi na hata mashabiki wake na inaweza kusababisha kufanya vibaya kwenye mechi za robo fainali.

Kwa sababu ligi inamalizika Mei 28 na michuano ya kimataifa inamalizika mwezi Juni, bado kuna muda wa kuangalia ratiba ya kuipachika tarehe ambayo haitokuwa na pilikapilika ya mechi za CAF.

HABARI KITAIFA

# ‘Tumieni taarifa za TMA kuongeza tija kimaendeleo’

**Na Ashton Balaigwa**, MOROGORO

SERIKALI imewahimiza wadau wa sekta mbalimbali na jamii, kutumia taarifa za hali ya hewa ili kuongeza tija na ufanisi kupanga na kutekeleza shughuli za maendeleo nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, wakati akifungua kikao cha siku mbili cha Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), mjini hapa.

Alisema serikali kwa kutambua umuhimu mkubwa wa Mamlaka hiyo, imeimarisha miundombinu na huduma za hali ya hewa nchini.

Aidha, inaendelea kufanya uwekezaji mkubwa wa kuimarisha mtandao wa Rada na miundombinu mingine ya hali ya hewa kama ilivyoainishwa katika Ilani ya uchaguzi ya CCM (mwaka 2020-2025).

Alisema, serikali imefanya na inaendelea na uwekezaji huo ambao ni hatua muhimu ya kuimarisha uwezo wa taifa katika kukabiliana na changamoto za matukio ya hali mbaya ya hewa na mabadiliko ya tabianchi kwa kuimarisha huduma za uangazi na utoaji wa tahadhari.

Alisema licha ya uwekezaji uliofanywa na kuendelea kufanywa na serikali, ni wajibu wa Mamlaka hiyo kuwa wabunifu katika kuongeza vyanzo vya mapato na kusimamia ukusanyaji wa mapato ili kupunguza utegemezi kwa serikali.

Naibu waziri pia, aliipongeza TMA kwa viwango vya usahihi wa utabiri ambavyo vinaendelea kuongezeka.

Naye Mwenyekiti wa Bazara la Wafanyakazi wa Mamlaka hiyo, Dk. Ladislaus Chang’a, aliishukuru serikali kwa juhudi kubwa ya kuwekeza katika miundombinu ya hali ya hewa.

Alisema maboresho na uwekezaji uliofanywa na serikali katika sekta ya hali ya hewa umechangia kuongezeka kwa usahihi wa utabiri kufikia wastani wa asilimia 88.3 kwa mwaka, kwa msimu wa vuli 2022 pekee usahihi ulikuwa asilimia 94.1.

Mwenyekiti wa Bazara la Wafanyakazi wa Mamlaka hiyo ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa alisema, hatua hiyo imechangia katika azma ya serikali ya kujenga na kukuza uchumi shindani.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Dk. Buruhani Nyenzi alisema, TMA imeendelea kufanya vizuri kwa kuwa katika kipindi chote cha uongozi taasisi imeendelea kupata hati safi ya ukaguzi wa hesabu.

Dk. Nyenzi alisema pamoja na mabadiliko ya uongozi wa TMA wa kustaafu kwa Dk. Agnes Kijazi, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu ambaye alihudumu kwa kipindi kirefu, bado Mamlaka imeendelea kusimama imara na kufanya vizuri katika nyanja zote za kitaifa na kimataifa.



Waziri Mkuu mstaafu John Malecela (kulia), akisalimiana na mmoja wa wachungaji baada ya kumalizika kwa ibada ya Pasaka, katika Kanisa la Angalikana Roho Mtakatifu Dayosisi ya Central Tanganyika, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Malecela ashauri sheria kali kupinga ushoga

**Na Peter Mkwavila,**

DODOMA

MWANASIASA nguli nchini Waziri Mkuu na Makamu wa Rais mstaafu, John Samwel Malecela, ameishauri serikali kuweka sheria ngumu na kali ikiwamo kifungo cha maisha kwa mtu yeyote atakayejihusisha na vitendo vya ushoga, ubakaji na ndoa za jinsia moja.

Malecela, alisema hayo baada ya ibada ya Sikuku ya Pasaka, kufufuka kwa Yesu Kristo iliyofanyika katika Kanisa kuu la Roho Mtakatifu Angilikana Tanzania, Dayosisi ya Central Tanganyika, jijini hapa.

Alisema, anasikitishwa na vitendo ambavyo baadhi ya watu wanavishabikia ikiwa ni pamoja na kujihusisha na masuala ya ushoga, ndoa ya jinsia moja na ubakaji.

“Mimi nawaomba Watanzania wezangu kulaani kabisa vitendo hivyo vya ushoga, ndoa ya jinsia moja na ubakaji kwa kuwa ni sehemu ya dhambi mbele za Mungu ambaye amekataza katika vitabu vyake vya dini na haiwezi kusameheka.

“Nitamshangaa sana Mtanzania yeyote ambaye ni mkristo anayeshabikia tabia hiyo ya ushoga wakati jambo hilo limelaaniwa na ushoga ni jambo la giza ni sawa na uchawi na ujambazi hivyo kuna kila sababu ya serikali kuweka sheria kali au kifungo cha miaka mingi kwa mtu yeyote ambaye atajihusisha na ushoga,” alisema malecela.

Naye Askofu wa Kanisa Aglikana Tanzania Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dikson Chilongani, aliwataka viongozi wa juu wa serikali kupambana na vitendo vya rushwa ambavyo vinaonekana kushamiri zaidi.

Alisema, nchi haiwezi kuwa na maendeleo ya kiuchumi kama haitapambana na kuzuia vitendo vya rushwa kwa kuwa dhami na inapotosha haki.

“Kwa hivi sasa rushwa inaonekana kushamiri kila mahali mahakamani, sehemu za utoaji wa huduma jambo ambalo linasababisha wanyonge kukosa haki zao za msingi na kuwanufaisha matajiri ambao wanatumia fedha zao,” alisema.

Aliwataka viongozi wa dini kutokutumia mahubiri kupotosha neno la Mungu kwa watu ili kuwaaminisha kwenye suala la miujiza badala ya kufanya kazi.

Alisema kuwa kwa sasa wahubiri wameanzisha injili za kuwaaminisha watu kuwa watapokea miujiza bila kuwaambia ukweli kuwa hakuna muujiza ambao unaweza kutokea kama mtu hajafanya kazi.

“Maandiko matakatifu yanafundisha wazi kuwa kila mtu afanye kazi na asiyefanya kazi asile, leo hii mtu anakuambia utapokea muujiza bila kufanya kazi hayo ni mahubiri ya upotoshaji.

“Israel ni nchi pekee yenye ukame mkubwa, lakini kwa sasa ni nchi pekee yenye teknolojia kubwa zaidi na hiyo inatokana na watu wake kufanya kazi kwa bidii na kuwa wabunifu zaidi.

“Nchi haiwezi kuwa na maendeleo kama itakuwa na watu wavivu, wazembe ambao wanategemea miujiza bila kufanya kazi ambayo itachangia kuongeza pato la taifa au mtu binafsi.

“Tatizo la uchumi wa nchi sio rais wa nchi au serikali yake, tatizo ni uvivu na uzembe wa wananchi wenyewe kwa kutopenda kufanya kazi ambazo zitawaingizia kipato cha uhakika,” alisema.

Aliwataka Watanzania kupambana na suala la ushoga na asiwapo mtu wa kuliunga mkono jambo hilo kwa kuwa ni chukizo mbele za Mungu.

Alisema suala hilo ni jambo ambalo wazungu wanataka kuliaminisha kwa mataifa ya Afrika ili kuendeleza laana ambazo Mungu alisha zitolea adhabu kama vile Sodoma na Gomora.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# CAG abaini serikali kupoteza trilioni 5/- mashauri ya kodi

**Na Godfrey Mushi,**
DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2021/22 imebaini mashauri 904 ya kikodi yaliyoko katika Mahakama za Rufani za Kikodi kwa muda mrefu yamesababisha serikali kukosa Sh. trilioni 4.84.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, CAG katika ukaguzi wake katika hesabu za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), alibaini kiasi cha Sh. trilioni 4.84 ni fedha walizozikosa kutokana na mashauri ya kikodi.

Mashauri hayo yanahusisha (Dola za Marekani 15,713,232 zilizobadilishwa kwa Sh. 2,292.733/Dola ya Marekani) kwa Tanzania Bara. Wakati Zanzibar, ilikuwa na mashauri 34 ya kodi yenye thamani ya jumla ya Sh. bilioni 3.43.

MAGARI YASIYOTUMIKA

Aidha, ripoti hiyo ilibaini pia kuna magari mabovu 547 yameegeshwa hadi Septemba 2022.

Alisema Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), ndio kinara wa magari mabovu, ambayo hayatumiki ambayo ni 86, Wizara ya Fedha na Mipango 51, Wakala wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA) 44, Wizara ya Mambo ya Nje 39 na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) 37.

Wakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Halmashauri ya Jiji la Tanga inaongoza kwa kuwa na 18, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu 15, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro 13, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa 12 na Mahakama ya Tanzania 23.

Yamo pia, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) 19, Wizara ya Afya 14, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) 176.

"Kuwapo kwa magari mabovu ya serikali ambayo yamehifadhiwa na hayatumiki kwa muda mrefu bila uondoshaji kulikuwa na athari zifuatazo ambayo ni, magari mabovu yaliyohifadhiwa na hayatumiki kwa muda mrefu huchakaa na huharibika zaidi na kwa kasi, na hivyo kupungua kwa kasi thamani yake, hata wakati serikali inapoamua kuyaondoa.

"Madhumuni ya ununuzi wa magari hayafikiwi ipasavyo, kwa vile magari hayafanyi kazi kulingana na madhumuni yaliyokusudiwa, kuongezeka kwa gharama za matengenezo kutokana na uchakavu wa magari mabovu ambayo yamehifadhiwa na hayatumiki kwa muda mrefu; na upotevu wa rasilimali-fedha za umma."

**500 YAUZWA**

Katika ripoti hiyo ya ukaguzi wa ufanisi, pia CAG alionyesha ukaguzi ulikokotoa tena thamani ya magari 500 yaliyotolewa, miongoni mwa magari yaliuzwa kwa watumishi wa umma, kuanzia mwaka wa fedha 2016/17- 2021/22.

Alibaini magari 482 sawa na asilimia 96.4 yalitathminiwa kwa thamani ya chini, huku tofauti hizo zikionyesha thamani ya magari 500 miongoni mwa yaliyochaguliwa yalitathminiwa kwa thamani ya chini sawa na Sh. bilioni 2.7.




Mjumbe wa Bodi ya Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (AMF), Abdalla Amour (aliyesimama), akionyesha kitabu cha juzuu pamoja na wanafunzi wa Madrasa ya Shifaiya Islamiyya, baada ya kuwakabidhi msaada wa vitabu 1104, mkoani Kaskazini Pemba jana, ikiwa ni mwendelezo wa utoaji sadaka wakati wa ibada maalum ya mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# AMF yakabidhi vitabu vya elimu ya dini Pemba

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya Asma Mwinyi Foundation (AMF), imekabidhi vitabu vya elimu ya dini (juzuu) 1,104 kwa wanafunzi wa madrasa ya Shifaiya Islamiyya iliyopo Kinyasini, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, ikiwa ni muendelezo wa sadaka wakati wa ibada ya mfungo wa Ramadhani.

AMF ambayo inajishughulisha na kuwasaidia wenye mahitaji maalumu hasa wanawake, wazee, watoto na wenye ulemavu, imekuwa pia ikitoa misaada mbalimbali katika nyumba za ibada, hospitali na jamii kwa ujumla. Akikabidhi msaada huo jana Zanzibar, Mjumbe wa taasisi hiyo Abdalla Amour, alisema wamekabidhi vitabu 1,104 katika madrasa hiyo yenye wanafunzi zaidi ya 150 kwa lengo la kuendelea kurithisha elimu ya dini kwa watoto na jamii ambayo itasaidia kudumisha utulivu katika nyanja mbalimbali.

"Urithi pekee kwa vijana wetu ni elimu ya dunia na dini, hivyo ni vyema wote kwa ujumla kushikamana na kuhakikisha jamii na watoto wanakuwa katika maadili mazuri ya kumjua Mungu, kwani hiyo itasaidia katika kupunguza mmomonyoko wa maadili kwenye jamii zetu," alisema Amour. Mwalimu Mkuu wa madrasa hiyo, Salama Juma Haji, aliishukuru Asma Mwinyi Foundation kwa kuwapatia vitabu hivyo, huku akibainisha kuwa wanakabiliwa pia na changamoto ya uchakavu wa majengo yanayotumika wakati wa kuwafundisha watoto.

"Katika madrasa yetu tuna vyumba viwili vya kufundishia, lakini kati ya hivyo kimoja hivi sasa hakitumiki tena kutokana na uchakavu, kimoja ndio kinatumika, inatulazimu nyakati ambazo sio za mvua watoto kutumia eneo la wazi kusomea," alisema Salama.

Naye Ustadh Amour Hamad Ali, alibainisha changamoto zingine wanazokabiliana nazo ikiwemo viti kwaajili ya wanafunzi na walimu, vifaa vya kufundishia ikiwamo misahafu na juzuu, na ukosefu wa majisafi, huku akitoa wito kwa wadau mbalimbali kusaidia kutatua upungufu huo.

"Elimu kwetu ni shida sana, leo 'jana' tunamshukuru sana Mungu kwa neema ambayo tumeipata kutoka kwa wenzetu hawa wa Asma Mwinyi Foundation kuja kutuona kwa upande wa juzuu, tunasema alhamdullillah Mungu awape moyo huo huo wa kusaidia," alisema Amour.

# Mtoto mwezi na nusu akutwa barabarani katelekezwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

MTOTO mchanga wa jinsi ya kike mwenye umri wa mwezi mmoja na nusu ameokotwa na wasamaria wema baada ya kutelekezwa na anayedaiwa mama yake katika mtaa wa Barabara ya Kawawa, Manispaa ya Lindi.

Mtoto huyo aliokotwa na Rehema Ally katika uwanja wa pembezoni mwa nyumba anayoishi, karibu na kituo cha mafuta, Machi 30, mwaka huu saa 2:00 usiku.

Akisimulia tukio hilo, alisema akiwa ndani ya nyumba anayoishi akiendelea na kazi yake ya kushona nguo, alisikia sauti ya mtoto mchanga akilia bila ya kubembelezwa.

Alisema kilio hicho kilichochukuwa cha muda mrefu, kilimshtua na kulazimika kutoka nje na kwenda nyumba kubwa kuwaita wapangaji wenzake waelekee anakolia mtoto huyo.

"Nilipofungua mlango namkuta mtoto pembezoni mwa ukuta wa nyumba tunayoishi kimeveshwa sweta kubwa na kutandikiwa nguo aina ya dera na kichwani kawekewa mtandio," alisema.

Alisema wapangaji wenzake walijitokeza akiwamo Juma Kilole na kutoa taarifa kwa Mwenyekiti wa mtaa wao, Hadija Selemani ambao kwa pamoja walimchukua hadi Kituo cha Polisi cha Wilaya kilichopo mjini Lindi.

Alisema baada ya ruhusa ya polisi mtoto huyo alifanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Sokoine na kubaini afya yake ni salama.

Aidha, aliwataka wanawake kuacha tabia ya kutupa watoto wanaowazaa kwa kuwa kwa kufanya hivyo ni kumkosea Mungu.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Sokoine, mkoani Lindi, Dk. Alexander Makalla, alithibitisha kumpokea mtoto huyo aliyeeleza ana uzito wa kilo tatu na kumfanyia uchunguzi wa kitaalamu ambaye alithibitisha ana afya njema.

Mkurugenzi wa Kituo cha Loving Heart Caring Hands, Mohamedi Chigogoro, alithibitisha kumpokea mtoto huyo Aprili 4, mwaka huu, kutoka kwa Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Lindi, Richard Kimaro. Alisema ni mtoto wa pili kupokewa na kituo hicho mwaka huu, hivi karibuni wamepokea mtoto wa kiume akitokea Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara na kufanya kiwe na idadi ya watoto wanne wanaoishi na kulelewa kituoni hapo.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Pilli Mande, alipoulizwa kupitia simu yake ya mkononi, kama taarifa ya kuokotwa kwa kichanga hicho, alisema yuko safarini hivyo hana taarifa.



# Taasisi yatoa msaada wa bidhaa, vyakula kwa wazee

**Na Allan Isack,** ARUMERU

TAASISI ya Smart Community on legal Protection imetoa msaada wa vyakula na bidhaa kwa wazee wa kituo cha Meru Elderly lnitiatives kilichopo Kata ya Kikatiti wilayani Arumeru mkoani Arusha.

Misaada hiyo ni sabuni, dawa za meno, nguo na vyakula ikiwamo kama vile sukari, mchele, unga wa mahindi na mafuta ya kupikia na kujipaka

Lengo la kutolewa kwa msaada huo kwa wazee hao wanaotunzwa majumbani na Kanisa la International Evangelism kwa kushirikiana na Shirika la Dorcas Aid International Tanzania ni kutambua mchango wao katika jamii wakati wa ujana wao.

Akizungumza jana wakati akikabidhi msaada huo, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Wakili Mary Mwita, alisema jamii unapaswa kuhakikisha wazee wanapata haki zao za msingi ikiwamo chakula na malazi kwa kuwa baadhi yao hawana uwezo wa kufanya kazi.

Alisema wazazi wamesaidia kwa kiasi kikubwa katika harakati za maendeleo ya kijamii na kwa nchi ujumla, hivyo aliwataka vijana wenye nguvu kuwatunza kwa kuwa kushindwa kuwasaidia ni kuchuma dhambi kwa Mungu kwa kuwa jambo hilo ni baraka kwa jamii na taifa.

Vilevile alisema suala la ukatili kwa wazee ikiwamo kuwanyima stahiki zao halikubaliki na aliwataka wadau wa haki za wazee kuwa mstari wa mbele kutetea bila kuchoka.

Alisema ni muda muafaka kwa wananchi kurudisha utamaduni wa kupeleka watoto kutembelea babu na bibi zao kwa kuwa utamaduni huo umekua ukisuasua ukilinganisha na miaka ya nyuma kwa kuwa sasa hivi kila mtu anamkumbatia mtoto wake.

Pia aliwashukuru wadau waliotoa zawadi kwa wazee na kulipongeza Kanisa la International Evangalism na Shirika la Dorcas kwa kuwajengea na kuwatunza wazee 10 na wengine 225 majumbani kwao.

Meneja wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Kanda ya Kaskazini, Vonness Koka, aliwashukuru wananchi kwa kuendelea kuwasaida wazee, akitoa rai kwamba ikiwezekana vituo vya kuwalea viongezwe kwa kuwa wazee wenye mahitaji yao ni wengi.

“Napata faraja sana kuona jamii inaona umuhimu wa kuwatunza wazee wetu, hatua hii inatukumbusha kuwa na sisi ni wazee watarajiwa, huenda tukaja kuhitaji msaada kama wao, kwa hiyo naishauri jamii isichoke kuwasaida na hata kama kuna uwezekano vituo vingi vianzishwe Ili kupunguza matatizo yanayowakabili,” alisema Koka.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa kituo hicho, Remigius Bonajose, alisema kituo hicho kina zaidi ya miaka 20 hadi sasa kinahudumia wazee 255 kutoka kata tano na vijiji nane vya Wilaya ya Arumeru.

Wakizungumza kwa niaba ya wazee wa kituo hicho baada ya kupokea msaada huo ,Fanuel Summary na Ndewaramisa Lazaro, walisema msaada umetolewa wakati muafaka kwa kuwa umeangukia Sikukuu ya Pasaka, hivyo watasherehekea kwa furaha.

Kadhalika, walitumia fursa hiyo kuwaomba wadau na wasamaria wema kuendelea kuwatembelea kituoni hapo mara kwa mara hata kwa ajili ya kuwapa salamu tu.

# Wajasiriamali 200 wapewa mafunzo ufugaji nyuki

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANAWAKE 200 wanaofanya shughuli za ufugaji wa nyuki wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wamepatiwa mafunzo na mizinga 120 ya kufugia nyuki ikiwa ni njia mbadala ya kuwakwamua kiuchumi, kukabiliana na umaskini.

Mafunzo na mizinga hiyo ilitolewa na Shirika la Tanzania People Wildlife (TPW), kwa ajili ya kuwasaidia wanawake hao kukuza uchumi wao pamoja na kujikwamua na wimbi la umaskini katika jamii.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa TPW, Neovitus Sianga, wakati akizungumza na wadau wa uhifadhi, wafugaji na viongozi wa vijiji na ngazi ya wizara.

Sianga alisema shirika hilo limefanikiwa kuwainua kiuchumi wanawake kutoka kwenye vikundi 100 katika eneo hilo, sambamba na kuwapatia mizinga 120 ya kufugia nyuki.

Mtaalamu huyo wa uhifadh, alisema ufugaji wa nyuki unaofanywa na kinamama hao umekuwa ukisaidia kutunza mazingira katika vijiji vyao.

Aidha, alisema shughuli wanazofanya zinasaidia kupunguza migogoro kati ya wafugaji na wakulima kwa asilimia, kadhalika ufugaji huo ukiwa sehemu ya kuwalinda wanyamapori.

Naye Chifu wa Mkoa wa Manyara, Alais Koina, alitumia fursa hiyo kutoa rai kwa wananchi kutunza mazingira, huku akiomba shirika hilo kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi sambamba na kuongeza watu katika mradi huo uwe endelevu.

Ofisa Usimamizi Nyanda za Malisho kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Alfred Mushy, alisema kwa kiwango kikubwa mabadiliko ya tabianchi yameharibu maeneo ya malisho.

Hata hivyo alisema wizara ilianza kuchukua tahadhali mapema kutokana na vifo vya mifugo vilivyosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.



Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mbulu, Anthony Lagwen (kushoto), akimbariki Mbunge wa Viti Maalum kupitia Vijana, Asia Halamga, baada ya misa ya Sikukuu ya Pasaka kwenye Parokia ya Mtakatifu Augustino, Katesh wilayani Hanang', mkoani Manyara jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanawake watakiwa kutumia matatizo yao kama fursa

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Dk.Suleiman Serera, amesema kuna umuhimu kwa wanawake ambao ni wadau wa madini ya tanzanite katika Tarafa ya Moipo wilayani humo kutumia matatizo yanayowakabili kama fursa kwa kutafuta mbinu mbadala ya kukabiliana nayo badala ya kulalamika.

Alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na wajasiriamali, wanunuzi wa madini, magonga, wauza maziwa, vyakula na matunda, ndani ya ukuta wa madini ya tanzanite uliko Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani.

Dk.Serera, alisema wanawake hao wanapaswa kubuni mbinu na njia mbadala za kuwatoa kwenye matatizo wanayokumbana nayo mara kwa mara na siyo kulalamika kila wakati.

“Wanawake ni jeshi kubwa hivyo mnapaswa kupambana kwa kuonyesha njia ya kuondokana na matatizo yaliyoko mbele yenu na siyo kulalamika juu ya vikwazo mbalimbali,”alisema Dk.Serera.

Aidha, alilipongeza Shirika la Civil Society Protection Foundation (CSP), kwa kufanya mdahalo na kuwakutanisha wadau wa madini ya tanzanite ili kutafuta mbinu za kuondokana na matatizo.


Mkurugenzi wa CSP, Nemency Iriya, alisema wameandaa mradi wa tanzanite na uchumi imara wa mwanamke ambao unaotarajia kuzinufaisha kata tatu za Mirerani, Endiamtu na Naisinyai. Mkurugenzi huyo alisema mradi huo umelenga kuhakikisha wanawake wajasiriamali wanaofanya biashara zao ndani ya ukuta unaozunguka migodi hiyo wanafanya kazi zao kwa ufanisi.

“Tunatarajia wanawake hao watafanya biashara zao kwa amani, uhuru na kwa faida kwa kuwa baada ya kujengwa ukuta unaozunguka migodi ya tanzanite, kumekuwa na changamoto zinazowakabili,”alisema.

Mmoja wa wadau hao, Mwanaidi Kimu, alisema wanawake wanaamriwa kuvua nguo za ndani na askari wa umri mdogo ili kupekuliwa na kusababisha ukatili wa kijinsia. “Japokuwa baadhi ya wanawake ndiyo wamesababisha hali hiyo kwa kufanya vitendo viovu kwa kuficha madini kwenye sehemu zao za siri ila tunaomba serikali iweke vifaa vya kutupekua,”alisema Kimu.

Naye Hawa Kiranga, alisema wanawake wajasiriamali wanaouza vyakula, matunda na maziwa, ndani ya ukuta hawaruhusiwi kutoa nje vinapobaki.

Alisema: “Tunaomba serikali ifanye mpango wajasiriamali waruhusiwe kutoka na vyakula vyao jioni endapo vikibaki ili watoto wao wakale nyumbani, kuliko kumwaga na kupata hasara”.





# Waiomba h'shauri ujenzi wa mitaro kudhibiti mafuriko

**Na Restuta Damian,** BUKOBA.

BAADHI ya wakazi wa Kata Bilele na Miembeni Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera wameomba Halmshauri ya Manispaa hiyo kusafisha mitalo inayopeleka maji katika Mto Kanoni yakitokea milimani ili kuepusha mafuriko katika makazi yao.

Wakazi hao waliwasilisha kero hiyo juzi wakati wakizungumza na Nipashe baada ya mfululizo wa mvua zinazoendelea kunyesha mkoani humo hususani katika eneo la Omkigusha, huku wakieleza kuwa hali hiyo itasaidia kudhibiti mafuriko yanayotokea mara kwa mara.

Mkazi wa Kata wa Bilele, Johansen John alisema, mvua nyingi inaponyesha hasa kipindi cha Aprili familia za mtaa wa Omkigusha hukumbwa na mafuriko na kusababisha familia kukosa mahali pa kuishi huku mali zao zikibebwa na maji.

Alisema ili kudhibiti hali hiyo mapema ni vyema halmashauri ifanye utaratibu wa kuzibua mitaro hiyo na kuruhusu maji kupita ikiwa ni sambamba na kupanua mto na kuongeza kingo ili kudhibiti athari za mafuriko.

Anod Jovin ni Mkazi wa Kata ya Miembeni alisema halmshauri isisubiri msimu wa mvua kuanza ndipo wapange ratiba ya usafi, kwamba ingekuwa hali ya mazoea kwa kila baada ya miezi kadhaa mitaro hiyo inasafishwa mafuriko yasingekuwa yanatokea. Akizungumza na Nipashe Ofisa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira, Innocent Buntuntu alisema mara nyingi shughuli za kibinadamu ndizo zimekuwa zikisababisha mafuriko katika makazi ya watu.

Buntuntu alisema halmashuri imekuwa ikitenga bajeti ya usafi wa mitaro kwa kuweka mkandarasi ambaye pia ushughulika na upanuzi wa kina cha mto na kusafisha mitaro hiyo, hivyo na msimu huu wanasubiri fedha ili waweze kuanza kutekeleza shughuli hiyo mapema.

"Tumeomba pesa ya kufanyia usafi wa Mto Kanoni unaopeleka maji kwenye Ziwa Victoria ili yasilete madhara ya mafuriko katika makazi ya watu japokuwa wapo wananchi ambao wanavamia maeneo hayo na kufanya ujenzi wa makazi kinyume cha sheria," alieleza

Kadhalika alisema kuendesha shughuli za kibinadamu katika vyanzo hivyo vya maji husababisha kuziba kwa mitaro sambamba na kufurika kwa mto hali inayosababisha mafuriko katika makazi ya watu.

# Serikali yajipanga kudhibiti utoroshwaji Kahawa

**Na Titus Mwombeki,** KYERWA.

SERIKALI wilayani Kyerwa mkoani Kagera imeanza kudhibiti utoroshaji wa kahawa kwa njia za magendo kwenda nchi jirani kinyume na sheria na utaratibu.

Akizungumza katika mkutano wa 36 wa chama cha ushirika cha Wilaya ya Karagwe na Kyerwa KDCU, Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa, Zaituni Msote alisema tayari wameanzisha kambi za muda katika maeneo ya mipakani zitakazo hakikisha zinadhibiti utoroshwaji wa zao hilo.

Msote alisema katika kipindi cha nyuma suala hilo lilikuwa limeshamili sana jambo ambalo lilikuwa likiisababishia serikali harasa kwa kupoteza mapato, hivyo kuwafanya kubuni mbinu zitakazo dhibiti tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kulinda mipakani pamoja na kwenye mihalo.

"Kambi hizo za muda tumeziweka katika maeneo yote ya mihalo katika Kata ya Mulongo, Bugomola, Kibale na Businde haya yote ni kupambana na wanaoendekeza tabia za kuuza zao hili nje kinyume cha sheria" alisema

Sambamba na hilo aliiomba KDCU kuzisaidia AMCOS zilizoko mipakani kwa kuwapa fedha zitakazo saidia kumudu soko la kahawa na kuepusha wafanyabiashara kuwa na fikra ya kufuata soko kimagendo katika nchi jirani.

Mbunge wa Karagwe na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa alisema kuwa tangu apewe jukumu la kusimamia KDCU matatizo yaliyokuwa yakichochea kufanyika kwa usafirishaji huo vitendo hivyo vimepungua ukilinganisha na ilivyokuwa hapo awali.

Alisema: "Tumeamua kutanguliza maslahi ya mkulima kwanza ndiyo maana mnayaona matunda haya lazima tushughulikie matatizo yote yanayowakabili wakulima pamoja na wafanyabiashara wa zao hili".




Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo (mwenye miwani), akifungua jiwe la msingi jengo jipya la kliniki ya mama na mtoto, lililojengwa kwa ufadhili wa watu wa Uholanzi katika Hospitali ya Misheni ya Kanisa Katoliki Dayosisi ya Mnero, kijiji cha Mnero Ngongo, wilayani hapo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Soko lakosa choo, W'biashara wajisaidia kwenye mifuko

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WAFANYABIASHARA wa Soko la Migombani lililopo wilayani Sengerema mkoani Mwanza wanalazimika kujisaidia katika mifuko nyakati za mchana kwa kukosa choo.

Inaelezwa kuwa nyakati za asubuhi soko hilo hutapakaa karatasi za plastiki pamoja na chupa zilizojaa haja ndogo pamoja na kubwa zinazotelekezwa baada ya wafanyabiashara kufunga shughuli zao.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wafanyabiashara wa soko hilo walisema kuwa kuna wakati wanalazimika kutafuta huduma hiyo katika makazi ya watu ambao hulazimika kulipia Sh.2,000 kwa mwezi ili waendelea kupata msaada huo.

"Tumekuwa tukikabiliana na mifuko yenye haja kubwa pamoja na mkojo kwenye makopo ya maji hali inayohatarisha afya zetu pamoja na wateja wetu, tunahitaji huduma ya choo ili hali ya usafi iwe imara katika eneo letu," alisema Sumai Kadi.

Katibu wa soko hilo, Richard Marko alisema kukosekana kwa choo katika soko hilo limedumu tangu Desemba 2021 mpaka sasa hawana huduma hiyo na tayari wamekaa na Mkurugezi wa Halmashauri ya Sengerema ili waweze kupata ufumbuzi.

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa Halmashauri ya Sengerema, Yanga Makaga alisema tayari amemuagiza Mkurugezi wa Halmashauri hiyo kutuma timu ya kufanya tathimini ya choo hicho ili wajue kinahitaji gharama kiasi gani ili waweze kukitengeneza na kuondoa adha hiyo.

Akieleza juhudi za walizozifanya katika kudhibiti hali hiyo kwa niaba ya Mkurugezi wa Halmashauri, Ofisa Elimu Shule za Msingi, Donalt Bunonusi alisema tayari wametenga fedha kwa ajiri ya ukarabati wa choo katika soko hilo.

Alisema zimetengwa Sh.milioni nne kutengeneza choo hiyo huku akiwaomba wananchi ambao wanafanya biashara katika soko hilo wawe wavumilivu wakati kikitengenezwa.

Nipashe
Spotika



GOLI LA MESSI UK. 14



DE BRUYNEY

HAALAND

# WACHEZAJI WA5 EPL WANAOLIPWA ZAIDI

**LONDON,** England

WACHEZAJI wa Ligi Kuu England ni baadhi ya wanasoka wanaolipwa fedha nyingi zaidi katika mchezo wa mpira wa miguu duniani. Ndio ligi maarufu zaidi ya soka duniani na ambayo hutafsiri kwa kiasi kikubwa cha mapato kupitia mikataba ya utangazaji na udhamini miongoni mwa nyinginezo.

Mishahara ya wachezaji ni kipengele muhimu cha soka la ndani. Ingawa ada za uhamisho mara nyingi huwa vichwa vya habari, vifurushi vya mishahara vikubwa vinavyotolewa kwa wachezaji vinaweza kuwa muhimu vilevile.

Mishahara mikubwa sio tu huvutia vipaji vya juu kwa klabu, lakini pia inaweza kuwa sababu ya kuamua katika uamuzi wa mchezaji kusaini timu mpya au kuongeza mkataba. Hata kama mchezaji anapatikana akiwa huru, anaweza kuwa na mahitaji ya juu ya mshahara ambayo yatazifanya baadhi ya timu kushindwa kumsajili.

Makala haya yanaangalia wachezaji watano wanaolipwa fedha nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu England msimu huu wa 2022-23, twende sasa...

**#5 Mohamed Salah (Liverpool) - Euro Milioni 1.7 kwa mwezi**

Mohamed Salah tayari ameingiza jina lake katika historia ya Liverpool na ni mmoja wa wachezaji wao bora wa zama za kisasa. Salah alivuka matarajio yote katika msimu wake wa kwanza kabisa katika klabu hiyo.

Katika msimu wake wa kwanza, Salah alipata mafanikio makubwa kwa kufunga mabao 32 katika michezo 38, na hivyo kuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya Ligi Kuu kufanya hivyo.

Tangu wakati huo amekuwa na jukumu muhimu katika ushindi wa Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu, Kombe la Carabao na Kombe la FA. Wekundu hao walimzawadia dili nono msimu uliopita wa joto ambapo nyota huyo wa Misri anapata mshahara wa euro milioni 1.7 kwa mwezi.

**#4 Jadon Sancho (Manchester United) - Euro Milioni 1.7 kwa mwezi**

Manchester United ilimsajili Jadon Sancho katika msimu wa majira ya joto wa 2021 kwa euro milioni 85.

Ni mchezaji wa nne kwa bei ghali zaidi katika historia yao. United walikuwa wanataka kusajili winga mwenye rekodi iliyothibitishwa na Sancho alikuwa amefanya kazi kubwa sana katika kipindi chake cha miaka minne akiwa na Borussia Dortmund.

Katika mechi 137 kwenye mashindano yote ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, raia huyo wa England alifunga mabao 50 na kutoa asisti 64. Alikuwa mmoja wa washambuliaji waliokuwa wakitafutwa sana wakati huo kutokana na sifa yake, Sancho alitarajiwa kupata mshahara mnono Manchester United.

United ililazimu na kumsajili kwa mkataba ambao ulimfanya apate euro milioni 1.7 kwa mwezi. Hata hivyo, usajili wa Sancho bado haujafaulu kwa 'Mashetani Wekundu' hao. Akiwa amefunga mabao 10 pekee na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 64 kwenye mashindano yote na hatma yake katika klabu hiyo bado haijafahamika.

**#3 David de Gea (Manchester United) - Euro Milioni 1.83 kwa mwezi**

David de Gea ni mmoja wa magolikipa bora wa enzi ya kisasa. Haikuwa muda mrefu uliopita kwamba alionekana kuwa mmoja wa makipa bora katika biashara. Raia huyo wa Hispania bila shaka alikuwa mchezaji bora wa Manchester United wakati wa miaka ya mwanzo ya enzi za baada ya Sir Alex Ferguson.

Alishinda tuzo ya 'Sir Matt Busby' kwa misimu mitatu mfululizo kuanzia 2013-14 hadi 2015-16. Thamani ya De Gea iliongezeka sana wakati huo na ilionekana kama angejiunga na Real Madrid mwaka 2015.

Hata hivyo, kwa misimu kadhaa ya hivi karibuni De Gea alikosolewa sana kwa kiwango chake hapo Man United. Lakini kutokana na mkataba wake wa sasa, ambao alitia saini Septemba 2019, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, anapata mshahara wa euro milioni 1.83 kwa mwezi.

**#2 Erling Haaland (Manchester City) - Euro Milioni 1.83 kwa mwezi**

Erling Haaland alikuwa mchezaji anayetafutwa zaidi katika dirisha la usajili la majira ya joto lililopita. Miamba kadhaa wa Ulaya ilijipanga kumsajili mshambuliaji huyo mchanga na hodari sana na Haaland alikuwa na chaguzi nyingi za kiwango cha juu za kuchagua.

Hatimaye aliamua kujiunga na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya England, Manchester City. Mshambuliaji huyo wa Norway anaweka mfukoni kitita cha Euro milioni 1.83 kwa mwezi na hicho ni kiasi cha fedha cha ajabu kwa mchezaji ambaye bado ana umri wa miaka 22 tu.

Tayari amefunga mabao 42 katika mechi 37 kwenye mashindano yote akiwa na Man City hadi sasa msimu huu.

Licha ya uvumi, mshahara wa Haaland uliokubaliwa na Man City hautavuka kiwango kilichokubaliwa na Kevin De Bruyne, ambaye sasa ana thamani ya karibu pauni 375,000 kwa wiki. Haaland amesaini kukaa na Man City hadi Juni 2027.

**#1 Kevin De Bruyne (Manchester City) - Euro Milioni 1.9 kwa mwezi**

Kevin De Bruyne amekuwa mchezaji bora katika Ligi Kuu England tangu kuwasili kwake mwaka 2015, akionesha kipaji chake cha ajabu kama kiungo. Amekuwa akiwavutia mashabiki, makocha na wachezaji wenzake kwa uchezaji wake wa kipekee, pasi sahihi na uwezo wa kufunga mabao muhimu.

Mchango wa De Bruyne kwa Man City umekuwa mkubwa, na amechukua jukumu muhimu katika mataji ya Ligi Kuu na mafanikio mengine ya ndani na Ulaya.

Uwezo wake wa ubunifu na kiwango cha kipekee cha kazi kwenye uwanja vimemletea tuzo na sifa nyingi binafsi, na hivyo kuimarisha hadhi yake kama mtu bora wa kisasa. De Bruyne ndiye mchezaji anayelipwa zaidi kwenye Ligi Kuu England, akipokea kitita cha euro milioni 1.95 kwa mwezi kama mshahara.

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Erling Haaland hadi sasa amecheza mechi 27 kwenye Ligi Kuu England na kufunga mabao 30 ambayo ni zaidi ya yaliyofungwa na Chelsea msimu huu. Chelsea mechi 30 mabao 29.





# WASHAMBULIAJI 8 VIWEMBE ZAIDI KATIKA HISTORIA YA UEFA

HAALAND

**LONDON,** England

KOMBE la Ulaya kwa Klabu ambalo sasa linajulikana kama Ligi ya Mabingwa Ulaya (Uefa), linachukuliwa kuwa moja ya mashindano ya soka yenye hadhi kubwa zaidi duniani kwa ngazi ya klabu.

Uwiano wa mabao kwa kila mchezo unatupa kipimo kizuri cha jinsi mshambuliaji yuko mbele ya lango. Kufunga mabao kwa wingi katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ndio jambo ambalo wachezaji wengi wanatamani kulifanya.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1955, mashindano hayo yameshirikisha klabu bora kutoka kote Ulaya na yametoa nyakati za kukumbukwa katika historia ya mchezo wa mpira wa miguu.

Wafungaji mabao au washambuliaji waliofanya vema kwenye mashindano hayo wanaheshimika na mashabiki na wachambuzi. Kuwa na rekodi nzuri katika Ligi ya Mabingwa kunaonekana kama alama ya ukuu wa kweli katika ulimwengu wa soka.

Haya sasa hebu tuangalie wachezaji nane bora walio na uwiano wa juu wa mabao kwa kila mchezo katika Ligi ya Mabingwa Ulaya...

**#8 Cristiano Ronaldo - Mabao 0.77 kwa kila mchezo**

Cristiano Ronaldo anatajwa na wengi kuwa mmoja wa wafungaji bora katika historia ya mchezo huo. Ustadi wake wa ajabu, uchezaji na umaliziaji umemfanya kuwa 'jinamizi' kwa mabeki katika mashindano hayo kwa miaka mingi.

Uchezaji wake mwingi na mabao yake ya ushindi yamemfanya apewe jina la utani 'Mr. Champions League,' akiimarisha nafasi yake kama mmoja wa wachezaji wakubwa kuwahi kupamba mashindano hayo. Akiwa na mabao 140 katika mechi 183, ana uwiano wa mabao wa 0.77 kwa kila mchezo.

**#7 Lionel Messi - Mabao 0.79 kwa kila mchezo**

Naam, hiyo hapo. Lionel Messi ana uwiano mzuri wa mabao kwa kila mchezo kuliko Ronaldo. Messi ni mmoja wa wachezaji waliofanikiwa zaidi katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na ameshinda shindano hilo mara nne katika maisha yake ya soka.

Messi ni wa pili kwenye orodha ya wafungaji bora wa muda wote wa Ligi ya Mabingwa. Ametikisa nyavu mara 129 katika mechi 163 kwenye shindano hilo. Mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or bila shaka ni mmoja wa wafungaji bora zaidi katika historia ya mchezo huo.

**#6 Robert Lewandowski - Mabao 0.82 kwa kila mchezo**

Robert Lewandowski ni mmoja wa washambuliaji bora wa zama za kisasa. Amekuwa katika kiwango cha ajabu cha ufungaji katika muda wote wa maisha yake, lakini alikuwa kwenye ligi ya aina yake katika misimu miwili iliyopita. Nyota huyo wa Poland alishinda Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya katika misimu miwili iliyopita.

Lewandowski, ambaye kwa sasa anachezea Barcelona, amefunga mabao 91 katika mechi 111 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#5 Alfredo Di Stefano - Mabao 0.84 kwa kila mchezo**

Alfredo Di Stefano alikuwa mwanasoka mashuhuri aliyeichezea Real Madrid kuanzia mwaka 1953 hadi 1964. Wakati akiwa na klabu hiyo, aliiongoza kushinda mara tano mfululizo Kombe la Ulaya, akifunga katika kila fainali.

Alijulikana kwa uhodari wake na uwezo wa kucheza nafasi nyingi uwanjani, pamoja na ustadi wake, maono na uwezo wa kufunga mabao.

Uchezaji wa Di Stefano katika Kombe la Ulaya ulisaidia Real Madrid kuwa kama moja ya klabu kubwa zaidi za soka katika historia. Gwiji huyo wa Real Madrid alifunga mabao 49 katika michezo 58 ya Kombe la Ulaya kwa kiwango cha mabao 0.84 kwa kila mchezo.

**#4 Jose Altafini - Mabao 0.86 kwa kila mchezo**

José Altafini ni mwanasoka mstaafu wa Brazil na Italia ambaye alikuwa na kiwango cha kipekee na klabu kadhaa bora nchini Italia na Brazil. Altafini alishinda Kombe la Ulaya mara mbili akiwa na AC Milan na alikuwa mfungaji mahiri katika mashindano hayo, akifunga mabao 24 katika mechi 28 pekee.

Ameiwakilisha Brazil na Italia katika ngazi ya kimataifa. Altafini pia anakumbukwa kwa uchezaji wake kwenye Kombe la Dunia la mwaka 1958, ambapo aliisaidia Brazil kushinda taji lao la pili la dunia.

**#3 Ferenc Puskas - Mabao 0.88 kwa kila mchezo**

Ferenc Puskas alikuwa mchezaji wa mpira wa miguu kutoka Hungary ambaye alikuwa na hadithi ya klabu yake na timu ya taifa. Anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora katika historia na mashine ya kweli ya kufunga mabao.

Katika Ligi ya Mabingwa, alifunga mabao 36 ya ajabu katika mechi 41 tu, ikiwa ni pamoja na mabao manne katika fainali ya mwaka 1960. Alikuwa mchezaji muhimu katika timu maarufu ya Real Madrid ya miaka ya 1950 ambayo ilishinda mataji matano ya kwanza ya michuano hiyo.

**#2 Gerd Muller - Mabao 0.97 kwa kila mchezo**

Gerd Muller alikuwa mwanasoka wa Ujerumani aliyeichezea Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ujerumani miaka ya 1960 na 1970. Anachukuliwa kuwa mmoja wa washambuliaji wakubwa katika historia na anajulikana kwa uwezo wake wa ajabu wa kumaliza.

Rekodi ya mabao ya Muller katika Kombe la Ulaya ni ya kuvutia, kwani alifunga mabao 34 katika mechi 35 pekee, yakiwamo mabao yake mawili katika fainali ya mwaka 1974 ambayo iliisaidia Bayern Munich kushinda Kombe lao la kwanza la Ulaya.

Muller pia alishinda mataji manne ya Bundesliga na Kombe la Dunia la mwaka 1974 akiwa na Timu ya Taifa ya Ujerumani, akiimarisha nafasi yake kama mmoja wa wachezaji wakubwa wa kizazi chake.


**#1 Erling Haaland - Mabao 1.32 kwa kila mchezo**

Ikiwa Erling Haaland anaweza kujiweka kama mfungaji bora zaidi katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mshambuliaji huyo wa Norway alijiunga na Manchester City msimu uliopita wa majira ya joto na amekuwa katika kiwango cha hali ya juu cha kuwafungia msimu huu.

Haaland ameonesha uwezo zaidi ya umri wake tangu msimu wake wa mapumziko (2019-20) akiwa na Red Bull Salzburg. Haaland amefanikiwa kufunga jumla ya mabao 33 katika mechi 25 tu za Ligi ya Mabingwa Ulaya hadi sasa katika maisha yake ya soka.

## Nukuu


"Alikuja baada ya kazi kunichukua. Alikuja akiwa na Bugatti wakati mwingine. Wenzangu walitupia jicho. Nilifika kwa basi na kuondoka kwa Bugatti," **Georgina Rodriguez, ambaye ni mchumba na mzazi mwenza wa nyota wa soka wa Ureno, Cristiano Ronaldo, akielezea namna uhusiano wao ulivyoanza na kuyafurahia maisha.**



"Binafsi, ningependa kumuona akimalizia soka lake akiwa Barcelona, Ulaya. Baada ya hapo, sijui atafanya nini. Messi lazima arejee Barcelona kwa ajili ya mapenzi ya soka na kwa sababu hakuondoka kama alivyopaswa kuondoka," **mshambulizi wa zamani wa Arsenal na Barcelona, Thierry Henry, akimtaka Lionel Messi kurejea 'Blaugrana' msimu huu wa majira ya joto.**



"Dini ni jambo langu binafsi, mimi ni muumini na tangu niliposilimu nadhani nilizidi kuwa na nguvu zaidi kiakili na kimwili, dini haikubadilisha utu wangu wala mtazamo wangu wa dunia, nasali mara tano kwa siku, naifanya hivyo kwa sababu inaniwezesha kuachiliwa na kujisikia vizuri baadaye," **mshambuliaji wa zamani wa Ufaransa na Bayern Munich, Franck Ribery**



Nipashe
Spotika



Kikosi cha Rivers United

# UKALI, UDHAIFU WAPINZANI SIMBA, YANGA CAF HUU HAPA

**Na Adam Fungamwango**

USIKU wa Jumatano iliyopita ilichezeshwa droo jijini Cairo, Misri na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), ambapo timu za Tanzania, Simba na Yanga zikapata wapinzani wao watakaomenyana nao kwenye michuano hiyo ya kimataifa kwa ngazi ya klabu barani humu hatua ya robo fainali.

Simba iliyo Ligi ya Mabingwa Afrika, itacheza na Mabingwa Watetezi, Wydad Casablanca ya Morocco, ikianzia nyumbani Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Aprili 21 na kwenda kumalizia ugenini Aprili 28, mwaka huu Uwanja wa Mfalme wa 5 jijini Casablanca.

Kwa upande wa Yanga inayocheza Kombe la Shirikisho barani Afrika, imepangwa kucheza dhidi ya Rivers United ya Nigeria, yenyewe itaanzia ugenini Aprili 23, Uwanja wa Godswill Akpabio kwenye mji wa Akwa, na itarudiana nayo Aprili 30, mwaka huu Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika makala haya, tutaziangalia timu hizi zitakazokutana na wawakilishi wa Tanzania, ukali, udhaifu, rekodi zao kwenye michuano ya kimataifa na ligi za nchi zinazotoka, ikiwa ni pamoja na njia ya kila timu hadi kufika hatua hiyo ya robo fainali.

Timu hizo pia zimeshawahi kukutana kwenye raundi ya kwanza na kila moja ikashika njia yake mpaka kufika hapo zilipo, haya sasa...

**#Wydad Casablanca (Morocco)**

Hawa ndiyo mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa walilolichukua msimu uliopita kwa kuichapa Al Ahly ya Misri mabao 2-0 kwenye mechi ya fainali.

Kwa sasa inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu nchini Morocco ikiwa na pointi 43, ikizidiwa alama nne na AS FAR inayoongoza kwa pointi 47.

Ilianza safari ya michuano hii msimu huu kwa kucheza dhidi ya Rivers United kwenye raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo ilichapwa mabao 2-1 ugenini Nigeria, kabla ya kupindua meza kibabe ikishinda mabao 6-0 nchini Morocco na kutinga hatua ya makundi.

Ilipangwa kwenye Kundi A na hadi inamaliza mechi zake sita ilikuwa kinara ikiwa imeshinda michezo minne, sare moja na kupoteza moja, mabao saba ya kufungwa ikiruhusu moja tu.

Timu hiyo imetwaa ubingwa wa Afrika mara tatu, 1992, 2017 na msimu uliopita, imelikosa kombe hilo mara moja baada ya kutinga fainali mwaka 2011, imetolewa mara mbili kwenye hatua ya robo fainali, 2018 na 1991, na imetolewa mara mbili hatua ya nusu fainali msimu wa 2019/20 na 2020/21.

Wydad pia imechua Kombe la Shirikisho mara moja 2002, na Super Cup linalochezwa na bingwa wa Ligi ya Mabingwa wa Afrika na wa Kombe la Shirikisho, mara moja 2018.

**#Rivers United (Nigeria)**

Timu hii ya Nigeria haina mafanikio makubwa sana kwenye soka la Afrika, huku rekodi zake zikionyesha kuwa iliishia raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2017.

Msimu uliopita ilikutana na Yanga kwenye mechi za awali Ligi ya Mabingwa Afrika na kushinda jumla ya mabao 2-0, ikifunga bao 1-0 mechi zote mbili nyumbani na ugenini, lakini iliondolewa kwenye raundi ya kwanza ikifungwa jumla ya mabao 2-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan, ikipoteza bao 1-0 ugenini, na kulazimishwa sare ya 1-1 nyumbani.

Mafanikio yao makubwa ni kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Mwaka 2017, ilipoishia raundi ya kwanza ilishuka kwenye Kombe la Shirikisho ikafanikiwa kutinga hatua ya makundi.

Msimu wa 2020/21, ilitolewa kwenye hatua za mchujo za Kombe la Shirikisho barani Afrika na ikakosa kuingia hatua za makundi ya kombe hilo.

Kwenye Ligi ya Nigeria ambayo inachezwa kwa makundi mawili, kwa sasa inashika nafasi ya tatu kwa pointi 19, kwenye Kundi B, linaloongozwa na Lobi Stars yenye pointi 20, Doma United nayo pia ikikamata nafasi ya pili ikiwa na pointi 20 zikizidiana mabao ya kufunga na kufungwa.

Kama ilivyo Yanga msimu huu, nayo ilianza kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Watanga FC ya Liberia hatua ya awali, ikashinda nyumbani mabao 3-0. Licha ya kupoteza kwa bao 1-0 ugenini lakini ilisonga mbele kwa jumla ya mabao 3-1 na kufanikiwa kutinga raundi ya kwanza.


Hapo ndipo ilipokutana na Mabingwa Watetezi, Wydad Casablanca ya Morocco, ikianzia nyumbani ikishinda mabao 2-1, lakini ikakutana na balaa ugenini nchini Morocco baada ya kubugizwa 6-0, hivyo kutolewa Ligi ya Mabingwa Afrika kwa jumla ya mabao 7-2, ikashuka Kombe la Shirikisho barani Afrika kwenye mechi za mchujo.

Ilijikuta ikiangukia mikononi mwa Al Nasr ya Libya kwenye upangaji wa droo, ikaanza mechi yake nyumbani Nigeria kwa ushindi mnono wa mabao 5-0, na kwenda ugenini nchini Libya kulazimisha sare ya bao 1-1.

Ushindi wa jumla ya mabao 6-1 ukaipa tiketi ya kucheza hatua ya makundi Kombe la Shirikisho, ikipangwa Kundi B ambalo ilimaliza ikiwa ya pili na pointi zake 10, nyuma ya ASEC Mimosas ya Ivory Coast iliyomaliza na alama 13.

Kwenye mechi sita ilizocheza, ilishinda tatu, sare moja na kupoteza michezo miwili.

## JE, WAJUA?



BAO alilofunga Lionel Messi wakati PSG ikiibuka na ushindi wa 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Ufaransa, 'Ligue 1' juzi dhidi ya Nice, linamfanya sasa kuwa mchezaji mwenye mabao zaidi ya 702 kwa ngazi ya klabu kwenye ligi tano bora barani Ulaya (Pemier League, LaLiga, Serie A, Bundesliga na Ligue 1), akimzidi Cristiano Ronaldo kwa bao moja. Lakini pia hadi sasa msimu huu katika mashindano yote, Messi amefunga mabao 19 na kutoa pasi za mwisho 'assists' 18 kwenye mechi 34 alizocheza.



# Walimu, wadhibiti ubora watakiwa kuhakiki vitabu shuleni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TEA), Dk. Aneth Komba amewataka walimu na wadhibiti ubora wa shule kuhakikisha vitabu vinavyotumika shuleni ni vile vilivyopata ithibati na siyo vinginevyo. Dk. Komba alisema hayo jijini Dodoma wakati akifungua mafunzo kwa walimu wa darasa la awali yaliyoandaliwa na Shirika la Children in Crossfire (CiC) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Dk. Komba alisema matumizi ya vitabu vilivyopata ithibati yatasaidia watoto kujifunza yale yaliyoandaliwa kwa ajili yao yakiwemo maadili ya kitanzania yenye kumjenga mtoto katika uelewa bora.

"Serikali inasisitiza matumizi sahihi ya vitabu vya ziada na kiada ambavyo vina ithibati, kuna utaratibu wa vitabu kupewa ithibati na Kamishna wa Elimu, kwa hiyo wanafunzi watumie vitabu ambavyo vimeidhinishwa na serikali,"alisema.

Katika hatua nyingine Dk. Komba aliwaelekeza wadhibiti ubora wa shule wakasimamie vyema utekelezaji wa mafunzo hayo ili kuhakikisha baada ya mafunzo hayo walimu wanakwenda kuboresha ufundishaji kwa wanafunzi wa darasa la awali.

"Mnapaswa mkakague na kuhakikisha kweli mwalimu anaandaa darasa changamshi,z ana za kutosha za kufundishia na watoto wanaweza kupata ule umahiri uliokusudiwa hasa za kusoma, kuandika na kuhesabu."alisema.

Mwakilishi wa Ofisa Elimu Mkoa wa Dodoma ambaye pia ni Mratibu wa Mradi wa Watoto Wetu Tunu Yetu, Lustica Turuka alisema ni matumaini ya Mkoa wa Dodoma kwamba baada ya mafunzo hayo walimu watapata mbinu mpya za ufundishaji wa darasa hilo.

Alisema hawataki tena utaratibu wa kufundishia watoto wa darasa la awali chini ya miti, kwamba kuanzia sasa watakwenda kuboresha madarasa.

Mwalimu wa darasa la awali kutoka Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Regina Masawe alisema mafunzo hayo yamemwezesha kupata nyanja nyingi za ufundishaji wa watoto wa darasa la awali.

# DUWASA yaombwa kupitia mapendekezo kupanda bei ya maji

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAKAZI wa mkoani Dodoma wameiomba Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) kupitia upya bei ya mapendekezo ya upandishaji wa bei za maji kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mapendekezo hayo ni bei ya kuanzia uniti sifuri hadi tano inayolipwa kwa hivi sasa ya Sh.1,170 hadi kufikia Sh. 1,632 ambazo zilipendekezwa kulipwa kwa mwaka wa 2025/26.

Mapendekezo hayo ya bei mpya yanayotakiwa kupitiwa upya na kufanyiwa utafiti wa kutosha ikiwamo yale ya mwaka 2023/24 ya Sh. 1,376 na ya mwaka 2024/25 ya Sh. 1,571 na Sh. 1,632 zilizopendekezwa kulipwa mwaka 2025/26 kwa wateja wa majumbani.

Wadau hao walibainisha hayo juzi jijini hapa, wakati wakitoa maoni yao kwenye mkutano wa kujadili bei mpya zilizopendekezwa na DUWASA, uliowashirikisha wananchi wa Jiji la Dodoma, Wilaya ya Chamwino, Kongwa Mji wa Kibaigwa na Wilaya ya Bahi. Vangiringa Murasi lisema kuwa bei hizo ni kubwa, hivyo DUWASA wanatakiwa kufanya utafiti wa kutosha ikiwamo maboresho ya miundombinu yao ili wateja wapate maji ya kutosha.

"Hatukatai kupandishiwa bei ya matumizi ya maji ila tunawaomba maboresho zaidi ya upatikanaji wa maji kwa kuwa bado kuna maeneo wadau maji wanayapata usiku wa manane tena sehemu zingine hayapatikani zaidi ya wiki nzima"alisema Vangiringa Murasi.

Awali akifungua mkutano huo Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule aliitaka DUWASA kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Maji ni huduma nyeti kwa uhai na ustawi wa wananchi na uchumi wa nchi yoyote ile na upatikanaji wake ni kielelezo tosha cha ubora wa maisha ya watu wote kwa ujumla"alisema

Alisema kuwa kwa mujibu wa sheria watoa huduma wanaodhibitiwa na EWURA kama Mamlaka ya Maji Dodoma, wana wajibu wa kutoa taarifa sahihi za utendaji wao kwa wateja wao na kwa kuwa jukumu lao la msingi ni kutoa huduma na bidhaa bora.

Alisema watumiaji wa huduma wanayo haki ya kupata huduma kwa wakati kwa bei halali, kuhoji ubora wa huduma wanazopata na kutoa malalamiko kwa watoa huduma na ikibidi kwa EWURA ili kero zote ziondolewe.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Nishati na Maji (EWURA), George Kabelwa alisema kuwa maoni hayo yatatolewa majibu yake kwa kushirikiana na Duwasa Julai mwaka huu. Mkurugenzi wa DUWASA, Mhandisi Haron Masawe alisema kuwa upandishaji wa bei hiyo ya mapendekezo utawasaidia kujiendesha kwa ufanisi zaidi.



Askofu wa Kanisa la Kiinjili na Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu akiendesha ibada ya sikukuu ya Pasaka, katika Usharika wa Dodoma mjini jana. Kulia ni Askofu Mteule wa Dayosisi hiyo, Mchungaji Christian Ndosa.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wasanii wapigwa marufuku kuchezea alama za dini

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

SHEKHE wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro, amepiga marufuku wasanii mkoani hapa kuacha tabia ya kuchezea alama za dini kwa lengo la kutafuta umaarufu.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waumini wa dini ya Kiislamu wakati wa dua ya hauli ya Shekhe Nassoro Issa Salum Alharith Alqadirii ambaye ni Baba wa Shekhe Issa Nassoro iliyofanyika kwenye Msikiti wa Muhajirina uliopo Majengo Manispaa ya Singida.

Dua hiyo iliyofanyika nyumbani kwake na kuhudhuliwa na viongozi wa juu wa dini hiyo mkoa iliendana na kufuturisha.

Shekhe Nassoro alisema iwapo kutakuwa na ujumbe ambao unatakiwa kufikishwa kwa wanawake inapaswa watafutwe wao na siyo watafutwe wanaume.

Alisema waislamu wanalaani kitendo kilichoonekana hivi karibuni kwenye mitandao ya kijamii wanawake wakionekana wakitangaza biashara, huku wakiwa wamevaa kanzu, kwamba kitendo hicho hakikubaliki.

Shekhe Nassoro alisema wakati vitendo hivyo vikitokea wameibuka baadhi ya wanasheria wakiwemo waislam ambao wanatetea wakieleza kuwa wanaovifanya wana haki ya kufanya na watahakikisha wanawatetea.

Aidha, aliwahimiza waislamu kujitokeza kumuunga mkono Mufti wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubeiry Bin Ali kwenye maandamano ya kupinga vitendo hivyo yatakayofanyika kuanzia Msikiti wa Masjid Taqwa hadi Stendi ya Zamani.

Mbunge wa Singida Mjini, Musa Sima alisema ujumbe alioutoa Shekhe Nassoro wa kupinga vitendo hivyo unapaswa kuungwa mkono na kuomba Aprili 16 iliyopangwa kufanyika maandamano ya kupinga vitendo hivyo hapa Singida wananchi wajitokeze kwa wingi.

Aidha, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na Mkoa wa Singida ukiwa ni mnufaika wa fedha hizo.

Pia aliwaomba waislamu kutumia Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na hata baada ya mwezi huo kuendelea kutenda mema ili Mkoa wa Singida uwe mfano kwa mikoa mingine.

Sima aliwaomba wananchi wa Mkoa wa Singida na mikoa mingine kumuombea kwa Mungu Rais Samia ili awe na afya na maisha marefu na kuendelea kuwaongoza Watanzania.





# Watu wenye ualbino waiomba jamii kuacha dhana, mila potofu dhidi yao

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WATU wenye ualbino mkoani Mbeya wameiomba jamii kuachana na mila potofu ambazo zinahatarisha maisha yao ikiwemo imani kwamba watu wenye maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi kupona endapo wakifanya mapenzi na wenye ualbino.

Mwenyikiti wa Chama cha watu wenye ualbino Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Claudy Mwakyoma alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na Nipashe kuhusu msimamo wao baada ya kuwepo kwa uvumi kwamba baadhi ya watu wanataka kufanya mapenzi na watu wenye ualbino ili kupona maradhi yanayowasibu.

Alipinga suala hilo na kusema ni imani potofu ambazo zinalenga kuhatarisha afya za kundi hilo ambalo mara kwa mara linaishi katika mazingira ya wasiwasi kutokana na mila potofu zilizojengeka kwa jamii.

"Kumekuwa na wimbi la mauaji dhidi ya watu wenye ualbino kutokana na imani potofu ikiwamo ukataji wa viungo, sasa kuna tatizo lingine kubwa limeibuka ambalo jamii inaaminishwa kuwa ukifanya mapenzi na mtu mwenye ualbino umepona UKIMWI jambo ambalo siyo kweli,"alisema.

Alisema mabinti katika kundi hilo wengi wao wameambukizwa maradhi na kupewa ujauzito hali ambayo imesababisha kuharibu ndoto zao na kuongeza wategemezi katika familia zao.

Aliongeza kuwa hakuna utafiti wowote ulifanywa kuhalalisha suala hilo na kuiomba jamii kuachana na imani hizo potofu ambazo zinazua taharuki na kusababisha kundi hilo kuishi kwa mashaka.

Bedason Mwaipyana mkazi wa Simike jijini Mbeya, alisema jamii inapaswa kuachana na imani za kishirikina kuhusu watu wenye ualbino kwa madai kuwa inasababisha kundi hilo kuwa na wasiwasi na kushindwa kufarahia maisha.

Aliiomba jamii kuzingatia misingi ya utu na haki za binadamu kama Katiba inayoelekeza sambamba na kutafuta riziki katika njia ya kumpendeza Mungu badala ya kutegemea imani za kishirikina ambazo zinaibua taharuki kwenye jamii.



Mwezeshaji wa Kituo cha kuhudumia waraibu wa dawa za kulevya cha Save Tanzania (SETA), Khalid Juma (kulia), akitoa maelezo kuhusu namna kituo hicho kinavyofanya kazi kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Nzonda Haki ambao ni wanachama wa Klabu ya Fema, jijini Mbeya juzi, waliotembelea kwa lengo la kutoa elimu ya Afya ya uzazi kujitambua na kuepukana na makundi hatarishi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Taasisi zatakiwa kutoa elimu ya uzazi, VVU kuisaidia jamii

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKURUGENZI wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Dk. Godlove Mbwanji amezishauri taasisi zinazotoa huduma za matibabu na huduma nyingine za kijamii, kuweka utaratibu wa kutoa elimu ya afya ya uzazi, maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na ujasiriamali ili kulisaidia kundi hilo kutimiza ndoto zao.

Dk. Mbwanji alitoa kauli hiyo juzi kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo zaidi ya watu wenye ulemavu 100 kutoka maeneo mbalimbali mkoani Mbeya.

Alisema kundi hilo limesahaulika sana jamii hususani kupatiwa elimu ya ujasiriamali na afya ya uzazi ambayo ingewasaidia kuamua na kupanga idadi ya watoto wanaowataka bila kujali hali walizonazo.

"Taasisi zinazotoa huduma za matatibu zinapaswa kulisaidia kundi hili kwa kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa huduma za afya ikiwamo kuajiri wakarimani kuandaa warsha mbalimbali za masuala ya UKIMWI na afya ya uzazi ili waweze kujilinda," alisema Dk. Mbwanji.

Alisema MZRH wataendelea kulisaidia kundi hilo katika nyanja mbalimbali ikiwemo kuwejengea uwezo ili kuweza kutimiza ndoto zao kupitia ujasiriamali sambamba na kulinda afya zao, tumekuwa tukifanya hivyo mara kwa mara kwa kulifikia kila kundi lakini awamu ya sasa tumeamua kuwaunganisha kuwapatia maarifa hayo.

Akifundisha masuala ya ujasiriamali mtaalamu wa elimu ya ujasiriamali ambaye pia ana ulemavu wa macho, Mwalimu Luca Mahenge alisema licha ya kundi hilo kusahaulika kwenye jamii lakini hakukata tamaa katika kutimiza ndoto yake.

Mahenge ambaye pia ni mwalimu wa shule ya Sekondari ya Ufundi Iyunga ya jijini Mbeya alisema alianza shughuli za ujasiriamali tangu akiwa darasa la saba ambapo alianzisha mradi wa ufugaji wa simbilisi.

Alisema katika kuhakikisha anatimiza malengo yake aliongeza bidii kwenye masomo huku akiendelea kufanya ujasiriamali ambao ulimwezesha kugharamia ada ya shule na maisha mengine.

## Waathirika dawa za kulevya kupewa elimu ujasiriamali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya vijana 1,000 kutoka taasisi mbalimbali za elimu mkoani Mbeya pamoja na waathirika wa dawa za kulevya wanatarajiwa kufikiwa na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Nzonda Haki ambao ni wanachama wa klabu ya fema. Lengo la kuyafikia makundi hayo ni kuwapatia elimu ya afya ya uzazi, kujitambua, ujasiriamali na uzalendo ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Miongoni mwa wanachama wa klabu ya fema shuleni hapo, ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha tatu, Glory Reuben alisema Shirika la Femina liliwajengea uwezo na namna wanaweza kuwa vijana bora kwa ajili ya kulisaidia taifa ambapo liliwajengea uwezo wa kujitambua na kufahamu mambo wanayopaswa kuyafanya kama vijana na uzalendo ambao utawasaidia kuishi kwa kusimamia misingi na maadili. "Baada ya kupata mafunzo hayo tuanzisha klabu ambayo imetuunganisha kwa ajili ya kufundishana masuala mbalimbali yanayohusu afya ya uzazi ikiwemo balehe na namna ya kukabiliana na vishawishi ili kutoharibu ndoto zetu kutokana na mimba pamoja tabia zingine ambazo zitasababisha kukatisha masomo yetu," alisema Glory.

Rojas Silungu mwanafunzi wa kidato cha pili, alisema kupitia klabu ya fema amejengewa uwezo wa namna ya kukabiliana na tabia hatarishi sambamba na kujiamini na kusimama mbele za watu kufundisha.

Alisema fema imekuwa msaada kwao kwani imewasaidia kujitambua kupata ujuzi na maarifa kwa kutumia fursa zinazowazunguka shuleni kwa kuanzisha miradi ya pamoja kama vile bustani za mboga ili kujiingizia kipato. Mwalimu wa klabu ya fema shuleni hapo, Yusuph Luziga alisema kwa sasa wana wanachama 180 kati yao wasichana ni 117 na wavulana ni 63.

Alisema katika kuhakikisha jamii inanufaika na klabu ya fema walianzisha utaratibu wa kutembelea vyuo na vijana walioathirika na dawa za kulevya wanaopata matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya.

Alisema: "Tumejiwekea malengo kuhakikisha tunayafikia makundi yote kwenye jamii yetu, kwa sasa tumeanza kwenye vyuo vikuu na vya kati tayari tulitoa elimu kwenye Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Chuo cha Maendeleo ya Jamii na Chuo cha Ufundi kilichopo eneo la Nzovwe, naamini kwa mwaka huu zaidi ya watu 1,000 tutawafikia," alisema Mwalimu Luziga.



## HABARI ZANZIBAR

# Bei za mafuta ya petroli, dizeli zashuka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BEI ya mafuta ya petroli Zanzibar imepungua kwa Sh.100 kwa Aprili kutoka Sh.2,880 Machi hadi Sh.2,780 kwa lita moja.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imetangaza bei hiyo jana ambapo kwa mafuta ya dizeli yamepungua kwa Sh.80 na mafuta ya ndege yamepungua bei kwa Sh.421.

Akitangaza bei za nishati hiyo ya mafuta kwa mwezi huu kwa waandishi wa habari, Kaimu Kitengo cha Uhusiano wa ZURA, Shara Shande Omar, alisema kushuka kwa nishati hiyo kunatokana na serikali kuendelea kufidia bei katika mafuta ili kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi.

Licha ya kushuka bei kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya ndege lakini mafuta ya taa bei ipo vilevile ya mwezi uliopita ambayo ni Sh.2,921 kwa lita.

Shara alisema mamlaka hiyo inapanga bei kwa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwemo kubadilika kwa wastani wa bei za uuzaji wa bidhaa hizo katika soko la dunia pamoja na soko la ndani kupitia Bandari ya Dar es salaam.

Hata hivyo, alisema pia ZURA inapanga bei kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani kwa mwezi uliopita ili kupata kianzio cha kufanyika mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi huu.

Aidha, alisema sababu zingine huangalia gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es salaam, huangalia thamani ya shilingi ya Tanzania kwa dola za kimarekani, gharama za usafiri, bima na premium hadi Zanzibar, kodi za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Shara alisema ZURA inaendelea kufuatilia na kudhibiti soko la mafuta na bei zake kwa ukaribu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha bei za bidhaa hizo haziongezeki na kutokea athari katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Aliwasisitiza wananchi kuwa bei hizo ndiyo bei halali na kuwahimiza kununua mafuta katika vituo halali na kudai risiti kila wanapopata huduma hiyo.

## Serikali yaanza kuzalisha vifaranga vya matango bahari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar chini ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeanza uzalishaji wa vifaranga vya matango bahari ili kuongeza kasi ya ufugaji wa mazao ya baharini.

Uzalishaji huo unafanywa na Taasisi ya Zanzibar Marine Hatchery, kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar na Kampuni ya AFRIVISON ambapo uzalishaji huo unafanyika katika kituo cha uzalishaji wa vifaranga vya samaki, kaa na matango bahari.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzalishaji huo, Mkurugenzi Mkuu wa Tasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini, Dk. Zakaria Ali Khamis, alisema tayari wameshazalisha vifaranga 2,000 vya matango bahari ambapo uzalishaji huo umechukua siku 45.

Alisema tayari vifaranga hivyo wameshavihamishia katika kitalu vilivyopo katika Bahari ya Kijiji cha Muungoni Mkoa wa Kusini Unguja ili kukua vizuri.

Mkurugenzi huyo alisema lengo la kuvitoa vifanga hivyo katika kituo cha kutotolea vifanya Betras na kuvipeleka katika kitalu cha bBahari ya Muungoni ni kuwazoesha mazingira halisi ya bahari na kuwa na makuzi mazuri.

Aidha, alisema eneo la Muungoni ni salama kwa makuzi ya vifaranga hivyo, ambapo vitaendelea kuhudumiwa ili viwe katika ukuwaji bora.

Hata hivyo alisema katika kuhakikisha kuwa malengo ya ufugaji wa matango bahari yanafikiwa kwa ufanisi mkubwa, hivi sasa wako katika mazungumzo ya mashirikiano na Nchi ya Madagascar kupata ujuzi zaidi wa uzalishaji wa vifaranga hivyo.

Wasimamizi wa vifanga hivyo katika kituo hicho, walisema licha ya kazi kubwa ya uzalisha vifaranga hivyo lakini wamejipanga kuhakikisha malengo ya serikali yanafikiwa na vifanga kuwa bora kulingana na soko la dunia.

Azizi Suleiman ni miongoni mwa wasimamizi hao, alisema uendeshaji wa shughuli za uzalishaji wa vifaranga katika kituo hicho unazingatia usalama wa kimazingira kwa kutumia vifaa vya kisasa pamoja na kudhibiti uingiaji wa bakteria katika eneo hilo la uzalishaji wa vifaranga.



Paroko wa Kanisa Katoliki, Parokia ya Mt. Joseph ya mjini Zanzibar, Padri John Mchomba (kushoto), akiwasha mshumaa wa Pasaka katika Ibada ya kubariki moto juzi usiku. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## Ukata wa fedha chanzo kumaliza migogoro ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar inakabiliwa na uhaba wa fedha kwa ajili ya shughuli ya utambuzi wa ardhi utakaosaidia kuondosha migogoro ya ardhi kwa wananchi.

Waziri wa wizara hiyo, Rahma Kassim Ali, alisema wizara yake ipo katika hatua ya kuomba fedha serikalini ili kuendelea na zoezi hilo la utambuzi wa ardhi ambapo kwa sasa limefikia asilimia 10.

Alisema asilimia hiyo imefikiwa kutokana na ushirikiano kutoka katika Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Waziri huyo aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati ya mawasiliano, ardhi na nishati na wenyeviti wa kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi na kuimarisha ushirikiano baina ya kamati hiyo.

Waziri Rahma alisema lengo la wizara ni kuyatambua maeneo yenye migogoro mingi zaidi ikiwemo maeneo ya uwekezaji na heka tatu zilizotolewa na Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume baada ya mapinduzi ya mwaka 1964.

Alisema utambuzi wa ardhi ni jambo muhimu na Zanzibar yote ikitambuliwa itawezesha kupunguza migogoro ya ardhi kwa asilimia 95 kwa sababu migogoro mingi inatokana na wananchi kukiuka taratibu za ardhi.

Hata hivyo, alisema wizara inachukua hatua ya kusikiliza migogoro kwa kuunda kamati maalum ya kusikiliza migogoro ya wananchi ambayo inakaa siku mbili kwa wiki.

Alisema tokea kuanza kwa kamati hiyo zaidi ya migogoro ya ardhi 170 imepokelewa ambapo kati ya hiyo ipo iliyopatiwa ufumbuzi, iliyopelekwa mahakamani na mingine inaendelea kufanyiwa kazi.

Akiwasilisha mada ya urasimishaji na usajili katika umiliki wa ardhi Zanzibar ,Mkurugenzi Idara ya Ardhi, Mtambua Hamziji Haji, alisema hadi sasa wameshatambua zaidi ya maeneo 50 Unguja na Pemba.

Alisema kuna changamoto kubwa ya watu kubadilisha heka tatu zilizotolewa na Rais wa kwanza wa Zanzibar baada ya mapinduzi kuwa makaazi ambapo maeneo hayo yalitolewa kwa ajili ya kilimo.

Alisema kuna faida kubwa ya utambuzi wa ardhi ikiwemo kuwa na uhakika na usalama wa haki ya matumizi ya ardhi, kupunguza au kumaliza kabisa migogoro iliyokuwepo na kuwezesha kumnyanyua mwananchi kiuchumi.

Mkurugenzi huyo alisema kwa mujibu wa taarifa za ufatiliaji na tathmini za MKURABITA mwaka 2008 hadi 2022/2023 ni kupungua kwa migogoro ya matumizi ya ardhi katika kipindi hicho ambapo zaidi ya migogoro 3,306 Zanzibar iliyotambuliwa na kutatuliwa.

Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati na wenyeviti wa kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi walisema kuna utoaji hati feki ambazo zinatolewa katika wizara na taasisi husika hali inayosababisha migogoro mingi ya ardhi Zanzibar.

# IBADA YA PASAKA KATIKA PICHA



Askofu mstaafu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Morogoro, Telesphor Mkude, akitoa baraka za kiaskofu kwa waumini baada ya kumaliza kuendesha ibada ya Pasaka katika Kanisa kuu la Mtakatifu Patrice, mjini Morogoro jana. **PICHA: JOHN NDITI**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akizungumza na waumini, baada ya kushiriki Ibada ya Pasaka katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**



Askofu wa Kanisa la ACTS Fellowship Tanzania, Dk. Mpeli Mwaisumbe akikemea ndoa za jinsia moja, wakati wa ibada ya Pasaka, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Wanakwaya wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, wakiimba wakati wa Ibada ya Pasaka, katika Usharika wa Azania Front, jijini Dar es Salaam., jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waumini wakishiriki Ibada ya Pasaka katika Kanisa Kuu Anglikana la Mtakatifu Albano, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 80 watekwa na wenye silaha nchini Nigeria

**ZAMFARA,** NIGERIA

KIKUNDI cha waasi wenye silaha wamewateka watu 80, wengi wao wakiwa ni wanawake na watoto katika jimbo la Zamfara nchini Nigeria eneo linalotajwa kuwa ni maarufu kwa matukio hayo.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya ndani, utekaji huo ulifanyika jana katika kijiji cha Wanzamai, na kuthibitishwa na wanakijiji ambao walisema waliotekeleza tukio hilo walikuwa wamejihami kwa silaha.

Msemaji wa polisi katika jimbo la Zamfara, Mohammed Shehu, alithibitisha tukio hilo, licha ya kutokutaja idadi kamili kwamba ni watu wangapi waliotekwa na watu hao wenye silaha.

Wakazi wa eneo hilo walisema, mpaka jana watekaji hao hawajaomba fedha ili kuwaachia huru raia waliowaweka kizuizini, ambao miongoni mwao ni kati ya umri wa miaka 12 hadi 17.

Inaelezwa kuwa watekaji katika jimbo la Zamfara na maeneo mengi ya Nigeria, huwa wanakaa na watu waliowateka kwa miezi kadhaa iwapo kikombozi hakijalipwa.

Hata hivyo inabainishwa kuwa kwa miezi kadhaa sasa, watu wenye silaha wamekuwa wakiwateka wananchi Kaskazini Magharibi mwa nchi hiyo, huku katika miaka ya hivi karibuni, vitendo hivyo vikitekelezwa na makundi ya kigaidi ya Kiislamu. **RFI**



Vikosi vya usalama nchini Israel vikiwa katika doria kwa lengo la kuimarisha usalama kutokana na uwepo wa matukio ya mashambulizi ya kushtukiza katika eneo la Ukingo wa Mashariki na Ukanda wa Gaza.
**PICHA:MTANDAO**

# Israel kukusanya wanajeshi na polisi wa ziada

**JERUSALEM,** ISRAEL

ISRAEL imeanza kuwaita polisi na wanajeshi wa akiba baada ya mashambulizi yaliyofanywa huko Tel Aviv karibu na Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kimabavu na kusababisha vifo vya watu watatu, akiwemo mtalii mmoja raia wa Italia.

Ilibainishwa kuwa licha ya kutolewa wito wa kutuliza mivutano, ghasia zimeongezeka tangu polisi wa Israel walipopambana na Wapalestina ndani ya eneo la msikiti wa Al-Aqsa katika mji unaopiganiwa wa Jerusalem wiki iliyopita.

Kwa mujibu wa vikosi vya huduma za dharura na polisi, raia huyo wa Italia aliuawa na watalii wengine saba walijeruhiwa katika shambulizi hilo, kabla ya mshambuliaji, dereva tax aliyetokea mji wa Kiarabu wa Kfar Kassem katikati ya Israel, kuuliwa na polisi.

Waziri Mkuu wa Italia, Giorgia Meloni, alimtaja mtalii huyo kuwa ni Alessandro Parini (36) na kwamba tayari polisi ya Israel imeanzisha uchunguzi wa wahusika wa shambulizi hilo.

Kutokana na shambulizi hilo, Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, aliwaagiza polisi kuwaita polisi wote wa akiba kutoka vikosi mbalimbali na kulielekeza jeshi kuongeza vikosi vya ziada.

Jeshi la polisi lilisema vikosi vinne vya akiba vya mpakani vimepelekwa katikati mwa jiji kuanzia jana na kuungana na polisi ambao tayari walikuwepo mjini Jerusalem na mji wa Lod, ambao una mchanganyiko wa Wayahudi na Waarabu.

Vuguvugu la Kiislamu la Hamas la Palestina, linalodhibiti eneo la Gaza lilielezea shambulizi hilo kama jibu la kawaida na halali kwa Isreal kutokana na hatua yake ya kuuvamia msikiti wa Al-Aqsa.

Taarifa kutoka Brussels, zilisema Umoja wa Ulaya (EU) umelaani mashambulizi hayo nchini Israel na kutoa wito wa pande zote kujizuia na kusitisha mashambulizi.

Mkuu wa sera za kigeni wa EU Josep Borrell, alikemea mashambulizi aliyoyaita ya kiholela ya roketi yaliyorushwa kutokea Lebanon na Ukanda wa Gaza.

"Tunaziomba pande zote kujizuia, kuzuia kushambulia zaidi kwa machafuko na kuhamasisha utulivu katika kipindi hiki cha sikukuu za kidini, hadhi ya mahala patakatifu ni lazima ilindwe," alisema Borrell.

**DW**

## Ukraine kuuza tena umeme nje

**KYIV,** UKRAINE

UKRAINE sasa imekuwa na uwezo wa kuuza umeme nje ya nchi kwa mara ya kwanza baada ya miundombinu yake ya nishati kurejea katika hali ya kawaida kutokana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Russia yaliyodumu kwa miezi kadhaa.

Rassia ilianza mashambulizi yake kwenye miundombinu ya nishati ya Ukraine Oktoba 2022, huku hali hiyo ikitajwa kusababisha mgawo na kukatika kwa umeme mara kwa mara na kuiacha miji mingi gizani wakati wa msimu wa baridi.

Aidha, inaelezwa kuwa hali hiyo ililazimu Ukraine kusitisha mauzo ya umeme nje, huku mamlaka za ndani zikibainisha kuwa kwa sasa zitakuwa na uwezo wa kuuza nishati ya ziada.

Waziri wa Nishati Herman Halushchenko, alibainisha kuwa alitia saini waraka wa kuidhinisha mauzo ya nishati nje, licha ya kwamba wateja wa ndani wanabaki kuwa kipaumbele.

Alisema mfumo huo umekuwa ukitoa uwezo wa ziada kwa karibu miezi miwili, na kwamba wananchi wa Ukraine hawakukabiliwa na upungufu tena.

"Kipindi cha baridi kali zaidi kimepita, hatua inayofuata ni kuanza kusafirisha umeme nje, ambayo itatuwezesha kuvutia rasilimali za ziada za kifedha kwa ajili ya ujenzi muhimu wa miundombinu ya nishati iliyoharibiwa," alisema Halushchenko.

Aliongeza kuwa kazi kubwa ya wahandisi na washirika wa kimataifa ni kurejesha mfumo huo.

Mwezi uliopita, miongoni mwa wakazi katika maeneo mengi ya Ukraine akiwemo Inna Shtanko anayeishi Dnipro aliiambia BBC kwamba vifaa vya umeme vilikuwa vya kutegemewa zaidi nchini humo.

"Sasa jiji limebadilika, mwishowe, taa za barabarani zinawaka, na haiogopeshi tena kutembea kwenye mitaa ya jiji," alisema Shtanko. **BBC**

## UN yasisitiza utawala wa kiraia Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN

MKUU wa Shirika la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, Volker Turk, ametoa tahadhari kutokana na hali ya wasiwasi nchini Sudan, akisisitiza pande zote kuzidisha juhudi zao katika kurejesha serikali ya kiraia.

Inaelezwa kuwa wanaharakati wa Sudan wanaounga mkono demokrasia waliandamana kupinga jeshi na wanamgambo wiki iliyopita wakati upinzani wa kiraia ukiadhimisha kumbukumbu kuu ya mapambano ya miongo kadhaa dhidi ya utawala wa kijeshi kwa maandamano mapya.

Vyombo vya habari vya ndani vilibainisha kuwa kuchelewa kwa mpango wa kusaini makubaliano ya kurejesha serikali ya kiraia nchini humo ambao ulipangwa kufanyika Alhamisi juma lililopita, ulisababisha upinzani wa kiraia kuitisha maandamano ya nchi nzima.

Turk, alizitaka pande zote kupunguza mivutano isisambae na kujiepusha na ghasia kwa kuwa hatua kubwa zimepigwa mpaka sasa ili kurejesha mageuzi ya kisiasa kwa njia sahihi. **VOA**

## HABARI MICHEZO

# MEYA DAR ANOGESHA FAINALI BETIKA MTOKO WA KIBINGWA

**Na Mwandishi Wetu**

MAMBO ni moto! ndivyo unaweza kutamka baada ya mamia ya mashabiki wa soka nchini wakiongozwa na Meya wa Kinondoni, Songoro Mnyonge, kushuhudia fainali ya Sodo Ligi ikiwa ni sehemu ya matukio ya amshaamsha ya Betika Mtoko wa Kibingwa.

Promosheni hiyo inawapa fursa washindi 100 wa Betika kuishuhudia 'dabi' ya Simba na Yanga itakayochezwa Jumapili kwa kukaa katika eneo la VIP, gharama zote zikiwa chini ya kampuni hiyo ya michezo ya kubashiri nchini.

Kwa zaidi ya miezi miwili, promosheni hiyo inayotoa mabingwa kila wiki imekuwa na amsha amsha sanjari na kuchezwa Ligi ya Betika Sodo iliyofikia tamati Jumamosi iliyopita kwenye fukwe za Coco, ikiongozwa na meya wa Kinondoni, Songoro Mnyonge, aliyeambatana na Meneja Mkuu wa Betika Tanzania, Samwel Laurence, ikiwa na kauli mbiu ya kuhamasisha usafi wa mazingira.

Katika fainali hiyo, 'vijana wa Amos Makalla' (RC FC) walishindwa kutamba na kuruhusu kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Sports Journalist iliyotwaa ubingwa na kuondoka na kitita cha Sh. milioni moja kama ilivyokuwa kwa 'dada' zao walioifunga Kopa G Queens bao 1-0.

Akizungumza katika fainali hiyo, Meya Songoro alisema imekuwa na hamasa kubwa na kuongeza amshaamsha ya Kampeni ya Mtoko wa Kibingwa inafanyika kwa msimu wa tano sasa.

Songoro pia ameipongeza Betika kwa kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kwenye michezo kwa kutoa zawadi ya pesa kwa washindi.

"Tunaona namna ambavyo Rais anahamasisha timu za Simba na Yanga kwa kutoa Sh 5,000,000 kwenye kila bao watakalofunga kimataifa na vinafanya vizuri, huku kwenye Sodo, Betika imeweka zawadi ya 1,000,000 kwa bingwa wa pande zote mbili, hii imeongeza hamasa, mshindi wa pili na watatu pia wameondoka na pesa," alisema na kuongeza:

"Baada ya fainali hii kuna mabingwa 100 wa Mtoko wa Kibingwa kutoka kote nchini watapata fursa ya kuishuhudia dabi Aprili 16 gharama zote zikiwa za Betika, hii inaonyesha namna Betika wamejitofautisha hatuna budi kuwapongeza,".

Meneja Mkuu wa Betika Tanzania, Laurence alisema fainali hizo ni sehemu ya amshaamsha kwa wateja wa kampuni hiyo tayari kuishuhudia dabi ya wakongwe wa soka nchini.

Alisema mabingwa wa Mtoko wa Kibingwa kutoka nje ya Dar es Salaam watawasili uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mwalimu Nyerere (JNIA), Jumamosi ijayo na kujumuika na wale wa Dar es Salaam tayari kuishuhudia dabi hiyo Jumapili.

"Kabla ya mechi ya dabi, kutakuwa na hafla ya bata la msimu pale Kidimbwi, mabingwa wetu pia watawasilikiliza wachambuzi mbalimbali wakiichambua dabi hiyo," alisema.

Ofisa Habari wa Betika Tanzania, Juvelinaus Rugambwa, alisema kampuni yao imetoa fursa kwa washindi 100 waliobashiri na kampuni yao nchini kuishuhudia dabi hiyo bure, gharama zote zikilipwa na Betika ikiwamo usafiri wa ndege kwa wale wanaotoka mikoani.

"Nafasi za kushinda zimebaki chache wiki hii, unachotakiwa ni kuweka beti tano za kuanzia Sh. 500 bila kujali mkeka umechanika au la unaingia kwenye promosheni ya Mtoko wa Kibingwa," alisema.




Meya wa Kinondoni, Dar es Salaam, Songoro Mnyonge (aliyevaa fulana ya njano katikati), akikabidhi cheti cha ushiriki kwa nahodha wa Sports Journalist FC, Mbwana Mshindo, baada ya timu yao kutwaa ubingwa wa Ligi ya Betika Sodo, ikiwa ni amsha amsha kuelekea dabi ya Simba na Yanga itakayochezwa Jumapili wiki hii. **MPIGAPICHA WETU**

# *Sputanza yataka wachezaji kuheshimu mikataba yao*

**Na Hadija Mngwai**

CHAMA cha Wachezaji wa Soka Tanzania (Sputanza), kimewataka kuhakikisha wanasoma na kueshimu mikataba yao pindi wanapoingia makubaliano na klabu yoyote ili kuondokana na utata pindi linapokuja suala la kuivunja.

Ligi Kuu Bara inatarajiwa kufikia ukingoni Mei 28, mwaka huu, na baada ya hapo dirisha jipya la usajili litafunguliwa, hivyo Sputanza limewaonya mapema wachezaji, likiwataka kuwa makini.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Sputanza, Mussa Kisoki, alisema ili kuondoa mikinzano baina ya wachezaji na klabu zao ni vema wachezaji wakaisoma na kuielewa mikataba yao kabla ya kuisaini.

"Kucheza mpira ni ajira kama zilivyo ajira nyingine, hivyo napenda kusisitiza kwamba wachezaji wasome mikataba kabla ya kusaini, pia waiheshimu ili iwasaidie kuwa huru pale wanapohitaji kuvunja.

"Wachezaji wanatakiwa kutambua kwamba mikataba wanayoingia na klabu ni ya kazi na ina kanuni zake ambazo zinalindwa na Fifa," alisema Kisoki.

Aidha, aliongeza kuwa kuna baadhi ya wachezaji huwa wanakuwa na tabia ya kwenda kujitibia majumbani mwao pasipo kupeleka uthibitisho katika klabu zao jambo ambalo ni kinyume cha taratibu.

Moja kati ya mvutano wa kimkataba uliopo kwenye Ligi Kuu kwa sasa ni kati ya Fesail Salum 'Fei Toto' na klabu yake ya Yanga, ambapo mchezaji huyo anahaha kutaka kuuvunja mkataba wake na klabu hiyo ikimtaka kufuata taratibu.

Fei Toto alitangaza kuvunja mkataba na klabu yake hiyo kwa kurejesha fedha za usajili katika akaunti ya Yanga, lakini klabu hiyo nayo ikazirejesha katika akaunti ya mchezaji ikimtaka kufuata utaratibu.

Hata hivyo sakata hilo liliamuliwa na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kuwa ni Fei Toto bado ana mkataba halali na Yanga, lakini mchezaji huyo ametia ngumu kurejea kuitumikia klabu hiyo.

# Baleke aanza ufalme Simba

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Simba raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Jean Baleke, amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi Machi wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, akianza kuwa mmoja wa wachezaji tegemeo na kipenzi cha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo.

Beleke ambaye usajili wake haukuwa na makeke sana kutokana na akili na mawazo ya mashabiki wa Simba kuwa kwa Cesar Manzoki, na ilionekana kuwa alisajiliwa baada kukosekana kwa mchezaji huyo, ameonekana kuwasahaulisha Wanasimba kila kitu kuhusu straika huyo mwenye uraia wa Jamhuri ya Afrika ya Kati akiwa na asili ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Mchezaji huyo amesema kufunga ndiyo kazi yake na hajaanza kufanya hivyo leo wala jana bali kwenye timu zote ambazo amepitia na hana wasiwasi kwa hilo.

"Nimefunga na nitafunga sana, hii ndiyo kazi yangu, nashukuru sapoti kubwa ya mashabiki wa Simba, na nimekuwa na bahati kubwa kwani hata kwenye klabu kadhaa nilizopita nilikuwa napata heshima kuwa kwao, na nimeshatungiwa hata nyimbo ninapocheza wanaziimba," alisema Baleke.

Hata hivyo, taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kupitia Idara ya Habari na Mawasiliano, ilisema kikao cha Kamati ya Tuzo za TFF kilichokaa Jumamosi, kimemchagua Baleke kuwa mchezaji bora baada ya kuonyesha kiwango kizuri kwa mwezi husika, akitoa mchango mkubwa kwa timu yake, ikiwa ni pamoja na kufunga mabao matatu kwenye dakika 81 alizocheza Simba ikiibuka na ushindi wa 3-0.

Alipachika 'hat-trick' hiyo Machi 11 kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro, Simba ikishinda mabao 3-0.

Aliwashinda Daruweshi Saliboko wa KMC na Jeremiah Juma wa Prisons kwa mwezi huo ambapo kila timu ilicheza mchezo mmoja.

Kamati hiyo pia ilimchagua Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, kuwa kocha bora wa mwezi, akiwashinda Nsreddine Nabi wa Yanga na Abdallah Mohamed 'Bares' wa Prisons.

Mpaka sasa ameshafunga jumla ya mabao 12, kiwamo 'hat-trick' mbili kwenye mechi zote alizocheza, akiwa amesajiliwa kipindi cha dirisha dogo akitokea Nejmeh SC ya Lebanon aliyokuwa akiichezea kwa mkopo kutokea TP Mazembe.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**TCHOUAMENI AWANIWA LIVER**
LIVERPOOL inajiandaa kwa msimu mpya, huku kiungo wa kati wa Real Madrid na Ufaransa, Aurelien Tchouameni, mwenye umri wa miaka 23, akiwa miongoni mwa ajenda zao kuu. (***El Nacional***)

**ZAHA ATAKIWA NEWCASTLE**
KLABU ya Newcastle na West Ham ndio walio mstari wa mbele kumsajili winga wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, mwenye umri wa miaka 30, kwa uhamisho wa bure wakati mkataba wake na Crystal Palace utakapokamilika msimu huu wa majira ya joto. (***Star***)

**DAU LA MCTOMINAY LATAJWA**
KLABU ya Newcastle Uited pia imekuwa ikivutiwa na Scott McTominay kwa muda mrefu, lakini Manchester United inataka angalau pauni milioni 50, kumuachia kiungo huyo wa kati wa Scotland mwenye umri wa miaka 26. (***Star***)

**OSIMHEN AGOMA KUONDOKA**
VICTOR Osimhen ameonekana kulengwa na Manchester United na Chelsea msimu huu, lakini mshambuliaji huyo wa Nigeria mwenye umri wa miaka 24, amesema ana furaha akiwa Napoli. (***France Football, via L'Equipe***)

**KANE NA MAN UNITED**
MATUMAINI ya Manchester United kumsajili Harry Kane msimu huu, yamechochewa na kusita kwa Bayern Munich kujihusisha na vita vya kuwania mchezaji huyo, huku Tottenham wakihitaji angalau pauni milioni 100 kwa mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 29. (***Mirror***)

**BAKU ATAJWA ARSENAL**
ARSENAL ina nia ya kumsajili beki wa Ujerumani na Wolfsburg, Ridle Baku, mwenye umri wa miaka 25, lakini itakabiliwa na ushindani kutoka kwa Chelsea na Villarreal. (***Caught Offside***)

**MARSCH MKATABA MPYA**
KOCHA wa zamani wa Leeds United, Jesse Marsch, amekubali mkataba wa muda mrefu kuchukua nafasi kama kocha Leicester City baada ya kukataa ofa ya Southampton Februari kwani walimpa dili hadi mwisho wa msimu. (Mirror)

**POTTER ANUKIA SOUTHAMPTON**
ALIYEKUWA Kocha Chelsea na Brighton, Graham Potter, anataka kuwa kocha ajaye wa Southampton, ikiwa watasalia Ligi Kuu England. (***Football Insider***)

**BARCA NA NYOTA WAKE**
BARCELONA iko tayari kutoa ofa kwa kiungo wa Hispania, Ansu Fati, mwenye umri wa miaka 20, winga wa Brazil, Raphinha, mwenye umri wa miaka 26 na mshambuliaji wa Hispania, Ferran Torres, 23. (***Sport***)

**ALLISTER LULU LIVER, CHELSEA**
LIVERPOOL na Chelsea watajaribu kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Alexis Mac Allister, mweye umri wa miaka 24 kutoka Brighton msimu huu. (***Relevo***)

**CLARKE AWINDWA PALACE**
KLABU ya Crystal Palace inamtazama winga wa Sunderland, Jack Clarke, mwenye umri wa miaka 22, kama mbadala wa Wilfried Zaha. (***Sun***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PEP: HAALAND NI DARAJA MOJA NA RONALDO, MESSI

**LONDON,** England

●●● Kipaji chake ni kizuri sana, kama mfungaji bora, tuliishi miongo miwili ya ajabu na...

PEP Guardiola anaamini Erling Haaland yupo daraja moja na Cristiano Ronaldo na Lionel Messi kama mfungaji bora baada ya mshambuliaji huyo juzi, Jumamosi kufunga bao lake la 44 msimu huu.

**Haaland alifunga mara mbili wakati Manchester City ikishinda mabao 4-1 ugenini dhidi ya Southampton na kuwasogeza ndani ya pointi tano dhidi ya vinara wa Ligi ya England Arsenal, ambao jana Jumapili walicheza dhidi ya Liverpool.**

Bao la pili la mshambuliaji huyo, lilimfanya afikishe mabao 44 katika michuano yote katika msimu wake wa kwanza nchini England.

Kati ya mabao hayo, 30 yamepatikana kwenye ligi, na Guardiola alijawa na sifa tele kwa Haaland baada ya ushindi huo, akilinganisha kipaji chake kikubwa na magwiji wawili wa soka, Ronaldo na Messi.

"Bao la pili lilikuwa la kushangaza," alisema Guardiola akiiambia BBC.

"Si rahisi kuokota mpira angani na kuuweka kwenye nyavuni.

"Kipaji chake ni kizuri sana. Tunamuhitaji. Kipindi cha kwanza hakikuwa kiwango chetu bora, lakini alibadilisha mchezo.

"Kama mfungaji bora, tuliishi miongo miwili ya ajabu na Cristiano Ronaldo na Lionel Messi, lakini yuko kwenye kiwango hicho. Anafunga mabao mengi."

Southampton, timu iliyo mkiani mwa Ligi Kuu, kwa kiasi kikubwa iliibana City katika kipindi cha kwanza hadi mpira wa kichwa uliogonga mwamba kutoka kwa Haaland ulipoweka mabingwa hao watetezi mbele dakika ya 45.

"Ninatoa sifa nyingi kwa Southampton. Mpango wao wa mchezo ulikuwa mzuri sana.

"Wakati mwingine unapaswa kutoa sifa kwa wapinzani wakati hauko kwenye kiwango chako. Tulibahatika kuwa mbele wakati wa mapumziko.

"Tulikuwa na ustadi zaidi katika kipindi cha pili. Tulipata bao la pili baada ya kushinda na baada ya kuwa rahisi."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 544
MECHI KALI
IHEFU FC
VERSUS
SIMBA
1 | 4.97
X | 3.53
2 | 1.64
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MESSI AFIKISHA MCHANGO WA MABAO 1,000

**PARIS,** Ufaransa

WIKI moja baada ya kukejeliwa na mashabiki wake, Lionel Messi, alifunga bao moja na kutengeneza jingine huku Paris Saint-Germain ikiifunga Nice mabao 2-0 na kurudisha uongozi wao wa pointi sita kileleni mwa Ligue 1 Jumamosi.

Messi alizomewa na baadhi ya mashabiki wa PSG katika mechi ya kichapo cha nyumbani dhidi ya Lyon wikendi iliyopita, na hivyo kusababisha uvumi zaidi kwamba anaweza kuondoka msimu huu wa majira ya joto.

Kwa bao lake la asisti, Messi sasa ana mchango wa mabao 1,000 katika maisha yake ya klabu, kwa mujibu wa takwimu za ESPN, kufikia hatua nyingine ya ajabu katika maisha yake ya soka.

Nyota huyo wa Argentina aliyeshinda Kombe la Dunia aliunganisha krosi ya beki wa kushoto Nuno Mendes dakika ya 26.

Kisha kona ya Messi kutoka upande wa kushoto ilifungwa kwa kichwa na beki mkongwe Sergio Ramos dakika ya 76.

Nice hawakufungwa katika mechi 14 kwa jumla kabla ya mchezo huo na walikaribia kusawazisha katika kipindi cha kwanza, lakini kipa wa PSG Gianluigi Donnarumma alizuia juhudi za Nicolas Pépé na mshambuliaji Terem Moffi.

Kombora la beki mkongwe Dante lilitoka chini ya lango na kuonekana kuvuka mstari dakika ya 51.

Lakini mwamuzi Jérémie Pignard hakuarifiwa na teknolojia ya mstari wa goli kwamba ilivuka, ingawa marudio ya video yalionyesha kwamba ni goli.

Donnarumma alizuia mikwaju mingi kutoka kwa Pepe na Youssouf Ndayishimiye huku Nice ikizidisha shinikizo kwa PSG, ambao wamepoteza mechi nane mwaka huu.

# Madrid yaisogezea ubingwa Barca

**MADRID,** Hispania

SAMU Chukwueze alifunga mabao mawili na kuleta pigo zaidi kwa matumaini ya Real Madrid kutwaa ubingwa walipolazwa 3-2 na Villarreal nyumbani kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumamosi licha ya kuongoza mara mbili.

Kikosi cha Carlo Ancelotti kilikuwa na matokeo mazuri walipowalaza wapinzani wao Barcelona 4-0 kwenye Uwanja wa Camp Nou katika nusu fainali ya Copa del Rey Jumatano.

Hata hivyo, hawakuweza kuendeleza kasi hiyo kwani waliangukia kwenye kichapo kilichowaacha na pointi 59 katika nafasi ya pili na kufungua milango kwa Barcelona kwenda kileleni kwa pointi 15 ikiwa wataifunga Girona leo Jumatatu.

Madrid wanaikaribisha Chelsea Jumatano katika mechi ya mkondo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ancelotti alikiri kwamba timu yake haikuwa na ari kamili Jumamosi.



"Ilikuwa ngumu kwetu kurudisha mpira, tulijaribu kushinda katika nusu yao, na hatukuwa na usawa," alisema. "Ndiyo sababu tuliruhusu mabao matatu.

"Kila mchezaji alikuwa na kiwango cha chini kuliko kawaida. Ilikuwa ngumu kuwa na motisha yetu kwa asilimia 100, juhudi dhidi ya Barca zilitugharimu. Hiyo ni kawaida, kushindwa huku kunaumiza, lakini sipendi kuzungumzia mtu binafsi.

"Haibadilishi hisia zetu kwa Jumatano, huo utakuwa mchezo tofauti kabisa. Ikilinganishwa na mwaka jana kwenye ligi, kiwango chetu kimeshuka."

Madrid walichukua nafasi ya mbele kwa dakika 15 baada ya krosi ya Marco Asensio kumpita Pau Torres wa Villarreal na kutinga wavuni kwa kujifunga.

Villarreal walipata bao la kusawazisha dakika ya 39 kupitia kwa Chukwueze, ambaye alikata ndani kutoka katikati ya eneo la hatari na kumshinda Nacho kabla ya kupiga shuti kali nje ya lango la Thibaut Courtois.

Vinicius alirejesha uongozi wa Real dakika mbili za kipindi cha pili kwa kumaliza rahisi mbele ya lango la Villarreal kwa bao lake la tisa la ligi msimu huu.

Vijana wa Quique Setien walisawazisha tena dakika ya 71 wakati safu ya ulinzi ya Madrid iliposhindwa kumzuia Jose Luis Morales aliyefunga kwa shuti kali.

Chukwueze alifunga bao lake la pili dakika 10 kabla ya mchezo kumalizika na kuwanyamazisha mashabiki wa nyumbani pale Santiago Bernabeu.

,830,140

JACKPOT

Lorem ipsum

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/04/23 | 22:00 | AC Milan vs Napoli | 2.64 | 3.08 | 2.59 |
| 02. 12/04/23 | 22:30 | San Lorenzo vs Boca Juniors | 2.75 | 2.65 | 2.49 |
| 03. 12/04/23 | 23:30 | Union Magdalena SM vs Deportivo Pereira | 2.23 | 2.95 | 3.21 |
| 04. 13/04/23 | 01:00 | Coritiba vs Sport Recife | 2.20 | 3.15 | 3.05 |
| 05. 13/04/23 | 01:00 | Belgrano Cordoba vs Huracan | 2.86 | 2.75 | 2.59 |
| 06. 13/04/23 | 03:30 | Rosario Central vs Independiente | 2.49 | 2.65 | 2.75 |
| 07. 13/04/23 | 03:30 | Estudiantes LP vs Atletico Tucuman | 2.20 | 2.91 | 3.32 |
| 08. 13/04/23 | 05:05 | Correcaminos Uat vs Club Celaya | 2.57 | 3.07 | 2.60 |
| 09. 13/04/23 | 19:45 | Feyenoord vs Roma | 2.24 | 3.14 | 3.19 |
| 10. 13/04/23 | 20:30 | Altay vs Altinordu | 2.18 | 3.12 | 3.02 |
| 11. 13/04/23 | 22:00 | Anderlecht vs AZ Alkmaar | 2.65 | 3.21 | 2.55 |
| 12. 13/04/23 | 22:30 | Colon Santa Fe vs Talleres | 2.65 | 2.80 | 2.44 |
| 13. 13/04/23 | 23:30 | Envigado FC vs Deportes Tolima | 2.75 | 2.70 | 2.46 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 10/04/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4310 | IFK Varnamo vs Mjallby | 2.42 | 3.12 | 2.66 |
| 15:30 | 2795 | Rosenborg vs Viking | 1.99 | 3.57 | 3.31 |
| 16:00 | 2536 | Kayserispor vs Umraniyespor | 1.90 | 3.57 | 3.57 |
| 16:00 | 2642 | AIK Football vs Norrkoping | 1.76 | 3.44 | 4.00 |
| 16:00 | 2671 | Reggina vs Venezia | 2.27 | 3.13 | 3.03 |
| 16:00 | 4094 | Osters IF vs Trelleborgs FF | 1.97 | 3.51 | 3.62 |
| 16:00 | 4813 | Jagiellonia vs Lechia Gdansk | 2.16 | 3.19 | 2.99 |
| 16:00 | 4815 | Vasteras SK vs Orgryte IS | 2.07 | 3.46 | 3.36 |
| 16:00 | 5138 | ASK Bravo vs Olimpija Ljubljana | 3.33 | 3.33 | 1.96 |
| 16:00 | 5318 | Ihefu FC vs Simba | 4.97 | 3.53 | 1.64 |
| 16:00 | 5417 | Varbergs Bois vs Elfsborg | 3.54 | 3.39 | 1.88 |
| 16:00 | 5543 | Kristiansund vs Fredrikstad | 1.59 | 4.10 | 4.21 |
| 17:00 | 1353 | Wigan vs Swansea | 2.75 | 3.20 | 2.42 |
| 17:00 | 2759 | Cardiff vs Sunderland | 2.60 | 3.11 | 2.60 |
| 17:00 | 3287 | Norwich City vs Rotherham | 1.51 | 3.94 | 5.79 |
| 17:00 | 3337 | Gazovik Orenburg vs Rostov | 2.09 | 3.44 | 3.13 |
| 17:00 | 3854 | Birmingham vs Stoke City | 2.75 | 3.10 | 2.48 |
| 17:00 | 4562 | Randers vs Copenhagen | 5.27 | 3.90 | 1.59 |
| 17:00 | 4577 | Coventry vs Watford | 2.36 | 3.16 | 2.86 |
| 17:00 | 4796 | Hull City vs Millwall | 3.00 | 3.20 | 2.25 |
| 17:00 | 5239 | Preston vs Reading | 2.04 | 3.36 | 3.31 |
| 17:00 | 5450 | Luton Town vs Blackpool | 1.48 | 3.95 | 6.20 |
| 17:00 | 5619 | West Bromwich vs QPR | 1.64 | 3.89 | 4.49 |
| 17:30 | 2381 | BSC Young Boys vs Grasshoppers | 1.33 | 5.02 | 7.53 |
| 17:30 | 5539 | FC Winterthur vs FC Luzern | 3.25 | 3.30 | 2.11 |
| 18:00 | 1875 | Tromso vs Molde | 3.57 | 3.57 | 1.90 |
| 18:00 | 2186 | Sarpsborg vs Bodo Glimt | 3.62 | 3.83 | 1.83 |
| 18:00 | 5103 | AFC Eskilstuna vs GIF Sundsvall | 2.03 | 3.51 | 3.41 |
| 18:00 | 5919 | Aalesunds vs Valerenga | 2.94 | 3.36 | 2.24 |
| 18:30 | 3666 | Radomiak Radom vs Rakow Czestochowa | 4.42 | 3.49 | 1.67 |
| 18:30 | 3994 | NK Mura vs NK Celje | 2.63 | 3.19 | 2.40 |
| 19:00 | 1140 | Cork City vs Dundalk FC | 2.68 | 2.94 | 2.52 |
| 19:00 | 1350 | Apoel Nicosia vs Apollon Limassol | 1.77 | 3.47 | 4.42 |
| 19:00 | 2870 | Pisa vs Cagliari | 2.37 | 3.08 | 2.92 |
| 19:00 | 4584 | Nordsjalland vs Brondby | 1.85 | 3.60 | 3.91 |
| 20:15 | 2659 | Brann vs Haugesund | 1.44 | 4.41 | 6.10 |
| 20:30 | 1820 | Sepsi Osk vs Rapid Bucuresti | 2.29 | 3.19 | 2.93 |
| 20:30 | 3137 | Fatih Karagumruk vs Fenerbahce | 4.41 | 4.04 | 1.64 |
| 21:00 | 1945 | Derry City vs Bohemians FC | 1.77 | 3.13 | 4.41 |
| 21:00 | 5648 | Jong Utrecht vs FC Oss | 2.10 | 3.28 | 3.18 |
| 21:00 | 5794 | Miedz Legnica vs Legia Warszawa | 4.74 | 3.66 | 1.60 |
| 21:45 | 3653 | Annecy FC vs Valenciennes | 2.15 | 3.20 | 3.20 |
| 21:45 | 3948 | Drogheda Utd vs St Patricks | 2.88 | 3.09 | 2.28 |
| 21:45 | 5676 | Shelbourne vs Sligo Rovers | 1.79 | 3.13 | 4.30 |
| 22:00 | 1401 | Barcelona vs Girona | 1.32 | 4.79 | 7.93 |
| 22:00 | 2135 | Shamrock Rovers vs UCD Dublin | 1.23 | 5.04 | 9.87 |
| 22:00 | 2445 | Burnley vs Sheffield Utd | 2.03 | 3.45 | 3.25 |
| 22:00 | 3347 | Sedan vs Nancy | 2.79 | 3.00 | 2.54 |
| 22:00 | 4536 | Alaves vs FC Andorra | 1.69 | 3.39 | 4.88 |
| 22:15 | 3702 | Gil Vicente vs GD Chaves | 2.00 | 3.21 | 3.66 |


# MVUA YA MABAO SIMBA YAZUA PRESHA AZAM FA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Kali Ongala, baada ya kuifuatilia Simba kwa makini dhidi ya Ihefu FC katika mchezo wao wa robo fainali wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC), maarufu Kombe la FA , amesema presha ni kubwa kuelekea mchezo wao wa nusu fainali.

Ijumaa iliyopita Simba ilifanikiwa kusonga mbele hatua ya nusu fainali ya ASFC kwa ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Ihefu FC, wakati Azam FC walicheza na Mtibwa Sugar na kushinda 2-1, mechi zote zilichezwa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Matokeo hayo sasa yanaifanya Azam FC kukutana na Simba katika hatua ya nusu fainali ya kombe hilo la Shirikisho la Azam, mechi hiyo ikitarajiwa kuchezwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ongala alisema ushindi wa mabao mengi Simba iliyoupta katika mechi iliyopita umewapa presha kubwa, hivyo wanarejea katika uwanja wa mazoezi kufanyia kazi madhaifu yao.

Alisema kazi kubwa waliyokuwa nayo mbele yao ni kukaa chini kufanyia kazi madhaifu yao na ubora wa wapinzani wao wajao (Simba) kuelekea mchezo wa nusu fainali.

"Ni kweli ushindi wa wenzetu (Simba), katika robo fainali umezidisha presha kubwa kwetu, kwenda kujipanga na kufanyia kazi mapungufu yetu na ubora wa Simba katika safu yao ya ushambuliaji ambayo inaonekana kuwa hatari," alisema Ongala.

Alisema wanatakiwa kujipanga vizuri zaidi na kutumia vema michezo yao ya ligi kutafuta ushindi ambao utakuwa ni sehemu ya maandalizi ya mchezo wa nusu fainali ya ASFC.

Aliongeza kuwa malengo yao makubwa ni kutwaa ubingwa wa Kombe la ASFC, baada ya kuukosa na kukata matumaini ya kubeba ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katika robo fainali nyingine, Yanga ambayo juzi usiku iliibuka na ushindi wa bao 1-0 kwa mbinde dhidi ya Geita Goold FC, sasa itakutana na Singida Big Stars hatua ya nusu fainali.

## KWAYA...



Wanakwaya wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani, wikiimba wakati a Ibada ya Pasaka, katika Kanisa la Azania Front jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Robertinho ataja silaha za ushindi*

INATOKA UK 24

"Nashukuru sana kwa kuchaguliwa kuwa kocha bora, kazi zetu za ukocha ni ngumu sana, siyo kitu rahisi tumecheza vizuri mwezi huu na kila mara nasema kazi hii mimi nafanya kwa ushirikiano na wenzangu, tunaamua kila kitu pamoja, ushirikiano mzuri wa benchi la ufundi na wachezaji ni muhimu sana kwenye timu," alisema.

Kocha Msaidizi wa Ihefu, Zuberi Katwila amesema wameyafanyia kazi mapungufu yaliyoonekana kwenye mechi iliyopita hasa kipindi cha kwanza ambapo Simba ilipata mabao manne.

"Kipindi cha pili tulirekebisha makosa yetu, tukacheza soka safi, nadhani tutaanzia tulipoishia," alisema.

Simba iko kwenye nafasi ya pili ya msimamo ikiwa na pointi 57, Ihefu nafasi ya sita na pointi zake 33.

Michezo
Nipashe Jumatatu Aprili 10, 2023



Madrid yaisogezea ubingwa Barca UK. 22

# Robertinho ataja silaha za ushindi

## ●●● Ni wakati Simba ikiivaa tena Ihefu leo kabla ya kuirudia Yanga na Wydad, asema...

**Na Adam Fungamwango**

SIKU mbili tu baada ya kukutana kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, timu za Simba na Ihefu zitaonyeshana tena kazi leo kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali mkoani Mbeya kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, huku Kocha Mkuu wa Simba Robertinho Oliveira, akitaja silaha zake za ushindi.

**Ijumaa iliyopita, timu hizo zilikutana kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), maarufu Kombe la FA, Simba ikiibuka na ushindi wa mabao 5-1.**

Hata hivyo, mechi ya leo inatarajiwa kuwa ngumu kwa Simba kwani Ihefu ina rekodi nzuri zaidi ikicheza kwenye uwanja wake wa nyumbani dhidi ya timu za Dar es Salaam msimu huu.

Novemba 29, mwaka jana ilibamiza Yanga mabao 2-1, ikaichapa KMC 1-0 Januari 3 mwaka huu, kabla ya kuidungua Azam FC bao 1-0 Machi 13, mwaka huu.

Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho, ameweka wazi kuwa hatopangua sana kikosi chake, badala yake ataweka 'nondo' zake zile zile, ingawa kutakuwa na mabadiliko kidogo ya hapa na pale.

Mechi dhidi ya Ihefu ya Ligi Kuu haitokuwa rahisi sana kwa sababu tuliwafunga mechi iliyopita, siwezi kubadilisha sana kikosi pamoja na kwamba tuna mechi kubwa tatu mbele yetu, kuna wachezaji sita ambao ndiyo msingi wa timu ni ngumu kuwabadilisha, ukiondoa hao tunaweza kufanya mabadiliko," alisema kocha huyo bila kutaja majina ya wachezaji hao.

Pamoja na hayo, kocha huyo amekiri uchovu wa wachezaji wake wengi kutokana na mfululizo wa mechi, lakini akaongeza kuwa ndiyo maisha ya wanamichezo duniani kote, huku akisifia kikosi chake kuwa kimebadilika sana na kinacheza soka la kuvutia, na kinachomfurahisha zaidi wameanza kuelewa kucheza bila ya kuwa na mpira.

"Tumechoka kwa mechi za mfululizo, lakini ni maisha yetu, mimi nikishirikiana na benchi langu la ufundi tumefanya kazi yetu vizuri na tukapata ushindi muhimu mechi zilizopita na hata dhidi ya Ihefu, pia kuna wachezaji wengine wameanza kuwa na uwezo mzuri na nitaweza kuwatumia hata kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa. Simba inacheza mpira mzuri sasa, ina staili yake ya uchezaji.

"Siku zote mpira mzuri unachezwa ukiwa huna mpira, na unapokuwa na mpira sawa, mtacheza mnapasiana mnakwenda mbele kutafuta mabao, lakini kama hamna mpira mnafanyaje? Hapo ndiyo kwenye umuhimu sana, uchezaji mzuri bila mpira ndiyo unaoipatia timu ya Simba matokeo kwa sasa, unaona tunashinda mabao matatu, manne, matano, sita mpaka saba," alitamba Robertinho.

Aidha, alishukuru kuchaguliwa kuwa kocha bora wa mwezi Machi, lakini akasema tuzo hiyo anaipeleka pia kwa kocha wake msaidizi, Juma Mgunda pamoja na benchi lake la ufundi kwani wamekuwa msaada mkubwa kwake.

INAENDELEA UK 23



Moja ya Silaha za ushindi za Robertinho Oliveira katika kikosi cha Simba, Jean Baleke, aliyeilaza Ihefu FC na viatu mechi iliyopita ya Kombe la FA, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi wiki iliyopita wakati wakilala 5-1.

# Kaze alia kiwango kibovu Yanga FA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema hajaridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na timu yake licha ya kupata ushindi na kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Kombe Shirikisho la Azam (ASFC), maarufu FA Cup.

Yanga imetinga hatua hiyo baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 kwa tabu dhidi ya Geita Gold FC, juzi katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili baada ya dakika 90 kutamatika juzi, Kaze alisema mechi ilikuwa ngumu kulingana na histori ya Geita Gold FC wanapocheza nao.

Alisema katika historia wanapokutana na Geita Gold wanakuwa na wakati mgumu, na kwamba msimu uliopita waliwatoa kwa mikwaju ya penalti na mchezo wa jana walikutana na ushindani mkubwa.

"Kipindi cha kwanza tulicheza chini sana, hatukuweza kutengeneza nafasi ya bao, lakini cha pili tulifanya mabadiliko ya kumuingia Mayele (Fiston) na kufunga bao moja hivyo kutuvusha kucheza nusu fainali," alisema Kaze na kuongeza:

"Licha ya kwamba tumepata ushindi na kusonga mbele, lakini sijaridhishwa na kiwango cha chini cha wachezaji walichokionyesha leo (juzi),"alisema kocha huyo.

Kocha huyo alisisitiza benchi la ufundi lina kazi kubwa mbele yao kwa kufanyia kazi madhaifu yao yaliyojitokeza katika mechi hiyo na kujianda na mechi zilizopo mbele yao ikiwamo michuano ya kimatifa.

"Wachezaji wanatakiwa kuwa makini, huu mwezi Aprili kuna ratiba ngumu, Jumanne tunacheza mechi ya ligi halafu tutakuja kujianda na mechi dhidi ya Simba na hiyo ni sehemu yetu ya maandalizi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika ," alisema Kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Geita Gold FC, Fred Felix Minziro, alisema mchezo ulikuwa wa ushindani mkubwa na kuwapongeza wachezaji wake kupambana na kutowapa nafasi Yanga kufunga idadi kubwa ya mabao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002